# UISLAMU
# NA
# MAFUNZO YA KIMALEZI

الإسلام والتعليم التربوية


**Kimeandikwa na:**
Sayyid Muhammad al-Qazwini

**Kimetarjumiwa na:**
Hemedi Lubumba Selemeni

**Kimehaririwa na:**
Sheikh Haroon Pingili

ترجمة

# الإسلام والتعليم التربوية

تأليف
السيد محمد القزويني

من اللغة العربية الى اللغة السوا حلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

**ISBN:** 978 – 9987 – 17 – 069 – 2

**Kimeandikwa na:**
Sayyid Muhammad al-Qazwini

**Kimetarjumiwa na:**
Hemedi Lubumba Selemeni

**Kimehaririwa na:**
Sheikh Haroon Pingili

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Agosti, 2014
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation

**S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ........................................................................ 1

Utangulizi wa chapa ya Pili ............................................................ 3

Utangulizi.......................................................................................... 4

Taratibu za Uzazi ............................................................................ 9

Chakula cha Mjamzito aliyeshikwa na Uchungu.......................... 10

Kumwonjesha (Tahniik) na Kumpa Jina....................................... 10

Akika................................................................................................ 12

Kuingia Sunna................................................................................. 13

Kunyonya......................................................................................... 14

Kuwabusu watoto, kuwakirimu na kuwalea ................................. 14

Silika ya Kujipenda......................................................................... 16

Mfumo wa Mtukufu Mtume (s) katika kutengeneza Jamii........... 17

Mwache mwanao acheze miaka saba ........................................... 21

Majukumu ya Wazazi katika Malezi ya Mtoto ............................. 23

Biashara na Kutafuta Riziki ya Halali ........................................... 26

Kuchagua kazi................................................................................. 27

Kilimo .............................................................................................. 28

Familia katika Uislamu................................................................... 29

Ndoa ........................................................................................31

Adabu za usiku wa kwanza wa fungate, na zile za kujamiiana ....35

Umiliki wa Ardhi na Uendelezaji wake ........................................41

Ujenzi wa Makazi .........................................................................43

Haki za Jirani ...............................................................................43

Usafi .............................................................................................44

Usafi wa Kinywa na Pua ..............................................................45

Kunyoa Nywele ............................................................................46

Usafi wa Mavazi ...........................................................................47

Dua na vigawanyo vyake .............................................................48

Dua ya Hamamuni .......................................................................50

Dua ya Mwenye kutoa Chafya......................................................50

Pongezi ya kupata Mtoto .............................................................51

Kumkirimu Mgeni .........................................................................51

Adabu ya Kula .............................................................................52

Kuchokoa Meno............................................................................54

Adabu ya Kunywa Maji .................................................................55

Safari na Adabu Zake...................................................................56

Tabia Njema za Safarini................................................................57

Barua na Mawasiliano........................................................................59

Urafiki ....................................................................................................59

Tabia Njema ...........................................................................................60

Ushauri na Kushauriana ........................................................................61

Haki za Wazazi wawili...........................................................................62

Uhalifu na Jinai .....................................................................................66

Adhabu ya zinaa: ...................................................................................67

Adhabu ya kulawiti: ..............................................................................67

Adhabu ya msaganaji, na kusagana: ......................................................67

Adhabu ya ukuwadi: ..............................................................................68

Adhabu ya kumtuhumu mtu kwa zinaa au ulawiti: ...............................68

Adhabu ya mwenye kumtusi Mtume, au Manabii
au Maimamu (a.s.): ................................................................................69

Adhabu ya mwenye kudai unabii: ..........................................................69

Adhabu ya mchawi: ...............................................................................69

Adhabu ya mlevi: ...................................................................................69

Adhabu ya mwenye kuhalalisha kilevi: .................................................70

Adhabu ya muuza pombe: .....................................................................70

Adhabu ya wizi: .....................................................................................70

Adhabu ya ugaidi: ........................................................................ 71

Mwenye kusulubiwa: ..................................................................... 71

Mwenye kufukuzwa na kupelekwa uhamishoni: ........................... 71

Adhabu ya mwenye kuritadi: ......................................................... 72

Adhabu ya kumwingilia mnyama: ................................................. 72

Kujitetea na kujilinda: ..................................................................... 72

Kisasi: ........................................................................................... 73

Aina za Uhai ................................................................................ 74

Marejeo ......................................................................................... 78

Bibiolojia........................................................................................ 81

بسم الله الرحمن الرحيم

## NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *Al-Islam wa Taalimul Tarbawiyyah* kilichoandikwa na Sayyid Muhammad al-Qazwini. Sisi tumekiita, *Uislamu na Mafunzo ya Kimalezi.*

Uislamu ni dini na ni mfumo kamili wa maisha haukuacha lolote linalomhusu mwanadamu kimwili au kiroho bila ya kuweka sharia za kuyaendesha maisha hayo (kiroho na kimwili).

Katika kitabu hiki mwandishi anaelezea kwa ujumla malezi, adabu na maadili ya Kiislamu kuanzia utotoni, ujanani, utu uzimani hadi uzeeni, na kuonyesha njia nzuri za kusoma na kazi za kufanya.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kwa hiyo, Taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu al-Hajj Hemedi Lubumba Selemani kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kwa Kiswahili kutoka lugha ya asili ya Kiarabu. Aidha tunawashukuru wale

wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI WA CHAPA YA PILI

**Bismillahi Rahman Rahim.**

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe wote. Rehema na amani zimwendee mbora wa viumbe wote, Bwana wetu Muhammad, na aali zake wema watoharifu.

Nimeandika kijitabu hiki kabla ya miaka saba, na Mwenyezi Mungu akataka kichapishwe na kutolewa, hivyo kikapata nafasi ya kuridhiwa na kukubaliwa na wasomaji. Tambua kuwa hakika mimi nilifanya kazi ya kukitunga na hali mimi kipindi hicho nimelazwa kitandani nikiwa mateka wa ugonjwa, hivyo sikupata nafasi ya kutosha ya kuhakiki mafunzo ya kimalezi yapatikanayo katika Qur'ani tukufu na katika Hadithi tukufu zilizopokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na kutoka kwa Maimamu miongoni mwa Ahlul-Baiti wake (a.s.).

Kijitabu hiki kikatoka na hali ni chepesi hakina uhakiki, uchambuzi na maelezo ya ziada. Ama leo baadhi ya ndugu wamejitolea kurudia kukichapisha Kijitabu hiki na wameniomba niandike utangulizi wa chapa ya pili, ndipo nimeandika mistari hii. Nawaombea na kujiombea mwenyewe kwa Mwenyezi Mungu taufiki ya ziada katika kuihudumia dini na akida, hakika Yeye ndiye mmiliki wa taufiki na ndiye aombwaye msaada.

Ameuandika Muhammad Kadhim Al-Qazwini
Rajab 1387 A.H.
Karbala Tukufu

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Muumba wa viumbe na Mgawaji wa riziki. Rehema na amani zimwendee mwalimu wa ubinadamu, mwokozi wa wanadamu dhidi ya giza za ujahiliya, Muhammad, na aali zake Maimamu waongofu na Masada walio viongozi.

Katika siku hizi za mwisho (za sasa) yamesambaa madai yenye sumu dhidi ya Uislamu na waislamu, na vimejitokeza vitabu vya upotovu na upotezaji na vimetarjumiwa na kukithiri katika nchi za Qur'ani (Kiislamu), na kwa maana hiyo kijana wa kiislamu amejitenga mbali na Uislamu wake, dini yake na hukmu zake.

Dhambi si dhambi yake yeye tu, kwani yeye huhifadhi ayasikiayo na hupokea kila anachopewa na mwalimu, na husawirika kichwani mwake yale ayasomayo muda wote wa miaka ya masomo yake, kuanzia hatua ya msingi hadi ya sekondari, ya juu hadi ya chuo kikuu, kipindi hicho hasikii chochote miongoni mwa misingi ya dini na hukmu za Qur'ani, mafunzo matukufu ya sharia ya kiislamu, wasifu wa viongozi wa Uislamu na historia ya waislamu, ila kitu kidogo mno.

Kwa sababu waandaaji wa selabasi za mafunzo na mitaala ya elimu, wameweka elimu za sayansi mahali pa Qur'ani, historia ya Wababiloni mahali pa maisha ya Manabii (a.s.), maisha ya Nabiljin mahali pa maisha ya Nabii wa Uislamu Muhammad (s.a.w.w.),

na mtazamo wa Darwin mahali pa mtazamo wa Uislamu juu ya ulimwengu, na mengine kama hayo.[1]

Hivyo basi ni nani mwenye kuulizwa kuhusu wanafunzi hawa, masikini waliohenyeshwa? Ni lini kijana wa kiislamu ataijua misingi ya dini yake? Ni katika nchi yake na ilhali hali ndio hii? Au katika nchi za Kimagharibi na Kimashariki ambazo ndio watu wenye uadui sana na Uislamu na waislamu?

Huenda msomaji ukastaajabishwa na neno hili, na ukalizingatia kuwa ni kali, lakini tambua kuwa hakika katika mwaka huu huu – nao ni mwaka 1380 A.H. – waislamu walitaka kununua ardhi huko London ili wajenge msikiti wao, lakini serikali haijawapa kibali cha kufanya hivyo!!!

Sikia hili na utazame wingi wa makanisa na shule za upadri zilizopo katika nchi zetu, nchi za Uislamu na Qur'ani. Hivi unataraji kijana wa kiislamu atajua chochote miongoni mwa misingi ya Uislamu katika nchi hizo?!!

[1] Ukiachia mbali mbinu hiyo pia katika ngazi ya jamii ya Kitanzania imezuka mbinu iliyojikita kwa mfumo mwingine uliojitambulisha kwa jina la Twisheni (*Tuition*), mfumo ambao umemnyang'anya kabisa mtoto wa kiislamu muda na wakati wa kuhudhuria mafunzo ya dini, ni wazi kwamba hapo kabla muda wa jioni na siku za mapumziko ya kiserikali ulikuwa unatumiwa ipasavyo na watoto wa kiislamu kwa kuhudhuria katika Madrasa kujifunza Qur'ani na taaluma zake, lakini kwa sasa mwanafunzi mwislamu au mtoto wa kiislamu hana muda tena wa kuhudhuria Madrasa, kwani sera ya twisheni imesisitizwa na kufanywa ndio msingi wa kufaulu mwanafunzi wa akademiki. Hivyo wazazi waislamu bila kujali aibu hii kubwa juu yao wamekuwa wakiwasisitiza watoto wahudhurie twisheni na kutoa pesa chungu nzima kwa ajili yake bila kutafakari hata kidogo muda wa nafasi ya Qur'ani na taaluma zake. Bali wako tayari kuwapeleka watoto wadogo shule za awali kwa gharama kubwa ya pesa na muda mwingi, lakini hawako tayari kuwapeleka Madrasa kwa gharama ya muda mchache tu. Amesema kweli Imam Ali (a.s.) aliposema: "Kauli ya haki lakini linalokusudiwa ni batili." Kwani ni kweli twisheni na masomo ya awali yana faida yakitumika ipasavyo, lakini si kwa mfumo huu tuushuhudiao ambao ni mbinu makhsusi ya kuwanyang'anya watoto wa kiislamu muda wa masomo ya Qur'ani na taaluma zake. –Mtarjumu.

Hii ndio selabasi ya wizara ya malezi na mafunzo au wizara ya maarifa (au wizara ya elimu na ufundi stadi) katika nchi za kiislam. Ama maelezo ya ufafanuzi ambayo yanatolewa na baadhi ya walimu pembezoni mwa vitabu vya kiada, ndio yaliyorithisha kwa mwanafunzi mwislamu fikra ambayo inamfanya aitazame misikiti kwa mtazamo wa dharau, na Qur'ani kwa mtazamo wa batili, na viongozi wa dini kwa jicho la dharau na istihizai, na hukmu za kiislamu na maelekezo ya kidini kwa mtazamo wa kuyakimbia na kukerwa nayo.

Neno la mwisho ambalo chuchu la ukafiri na shirki – chuchu la ukoloni na uadui – umeliweka katika kinywa cha waislamu ni neno hili: Uislamu ni dini ya ibada tu: Yaani ni dini ya Swala, Swaumu na Hija tu, wala hauna uhusiano wowote na uchumi, wala ujuzi wa utamaduni na maendeleo, wala hauna elimu ya tiba na hekima, wala ujuzi wa mambo ya viwanda na kilimo, hauna maarifa ya nyota na maumbo, falaki na sayari, wala hauna mafungamano na chochote miongoni mwa mambo ya maisha, nidhamu ya kijamii na ya mtu mmoja mmoja.

Ndio, ni haki kwa hawa masikini majahili kukubali neno hilo kali iwapo nafsi zao zitaafiki, mpaka wamekuwa wakilitumia kufanya istihizai. Ni haki kwa hawa kukubali na kunyamaza au kushindwa kuutetea Uislamu wao uliotukuka, kwa sababu wao wako mbali na kila kitu kinachoihusu dini, hivyo hakuna budi neno la uzushi na tuhuma juu ya Uislamu liwaathiri, Uislamu ambao ndio dini bora na sheria nzuri mno.

Hakika ujahili wa kutokujua misingi ya Uislamu na kutokujua mema yatokanayo na kushikamana na dini, upande mmoja vimekuwa ni sababu ya madai hayo na kuathiriwa na tuhuma hizo. Na upande mwingine ni kwamba sifa chafu zimeanza kutapakaa kati yao, kama vile uongo, khiyana, unywaji wa pombe na kutenda

maasi, kuenea kwa dhuluma, ulaghai katika miamala yao na mengineyo mengi.

Kujitenga huku kumeonyesha jinsi sura ya Uislamu na Qur'ani ilivyochafuliwa, na pia sura ya viongozi wa dini kuanzia Mtukufu Mtume, Maimamu watoharifu hadi ulamaa, hivyo watu baki – Mayahudi na Manaswara na wafuasi wa dini nyingine – wakadhani kwamba hakika dini ya Uislamu ni dini ya uongo na khiyana, dini ya dhulma na ujeuri, dini ya riba na zinaa, dini ya pombe na kamari, dini ya kila chafu na ya kila sifa mbaya, kwa sababu kila mwenye dini huwakilisha dini yake. Na mtu atakapo kuijua misingi ya dini yoyote ile anaweza kufahamu hilo kupitia mfuasi wa dini hiyo, kwa sababu yeye ni mfano wa dini yake na sura ya imani yake. Wala hao watu baki hawajajua kwamba aibu na nakisi ipo kwa waislamu na si katika Uislamu.

Nyakati hizi za mwisho, mmoja wa wanafalsafa wa Kimagharibi ameyaona baadhi ya mazuri ya Uislamu, fadhila zake na faida zake, hivyo akaandika kitabu kuhusu Uislamu na akakihitimisha kwa neno hili: "**Uislamu ni kitu baki, na waislamu ni kitu kingine**."

Ndio, haki na ukweli ni kwamba Uislamu ni dini ya kila la kheri, dini ya maisha na ustawi, dini ya ustaarabu na maendeleo, dini ya upendo na umoja, dini ya elimu na uhuru, dini ya imani na uaminifu, dini ya sharafu na fadhila, dini ya haya na utawa, na mwisho ni kwamba Uislamu ni dini ya kila sifa nzuri, ni dini ya tabia zote njema na sifa nzuri.

Hakika Uislamu ni dini kamili iliyotimia inayohusu kila kitu, imekiwekea kila anachokihitaji mwanadamu kanuni na hukumu, maamrisho na makatazo, ili kudhamini wema wake katika maisha. Kanuni hizo zinajumuisha anayoyahitaji mwanadamu kabla ya kuumbwa kwake katika tumbo la mama yake na mpaka kuzaliwa

kwake, pia anayoyahitaji katika hatua na mizunguko ya maisha yake mpaka kufa kwake na mpaka kuwemo kwake kaburini. Dini hii haihusiki na ibada tu bali ibada ni moja tu ya maeneo ya kanuni hizo.

Ewe msomaji laazini! Hivi sasa punde tu utaingia ndani ya uchambuzi wenyewe, ili uujue Uislamu kama ulivyoteremka na si kama tuuonavyo leo, ili uujue Uislamu kama alivyoutambulisha Mwenyezi Mungu, Mtume wake na Maimamu watoharifu (a.s.), na si kama walivyoutambulisha leo baadhi ya waislamu kwa vitendo vyao. Itakubainikia hivi karibuni jinsi gani waislamu wamenyimwa utajiri wa kielimu wa kiislamu na pia madini ya baraka na hazina za kheri na wema, hayo yote ni kutokana na kutoifahamu vilivyo dini yao, au ni kwa sababu ya kupuuzia kwao mafunzo ya Uislamu wao.

Hebu hivi sasa tujaalie mtoto kazaliwa toka tumboni mwa mama yake, naye baada ya kujitenga na mama yake bado yuko juu ya ardhi, tutake sasa kutekeleza juu yake mafunzo ya kiislamu, kisha tuwe pamoja naye mpaka afikie utu uzima.

Hivyo hapa sasa tunataja sehemu ndogo tu ya mambo ambayo yanahusu maisha yake upande wa sekta zote na nyanja zote na katika mambo mbalimbali, lakini hatutataja ibada wala yanayoihusu tiba, kwa sababu nafasi ni finyu nasi tupo katika kutaja na kutoa muhtasari, na kwa sababu ulamaa wetu wameandika vitabu vingi kuhusu tiba, mfano tiba ya Nabii, tiba ya Maimamu, tiba ya Imam as-Sadiq na tiba ya Imam Ridha. Hivyo hebu sasa tuiendee dini ya Uislamu ili tusikie yasemaje kuhusu haki ya mtoto huyu.

Muhammad Kadhim Al-Qazwini
Karbala
1380 A.H.

بسم الله الرحمن الرحيم

## TARATIBU ZA UZAZI

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "…..na kumwogesha mtoto aliyezaliwa ni lazima."[2]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Mambo saba ni Sunna kufanyiwa mtoto anapozaliwa: La kwanza ni kupewa jina. La pili ni kichwa chake kunyolewa. La tatu ni kumtolea sadaka ya sarafu kwa kiwango cha uzito wa nywele zake, au dhahabu yenye thamani ya sarafu hizo. La nne ni kufanyiwa akika. La tano ni kichwa chake kupakazwa zafarani. La sita ni kufanyiwa tohara kwa kutahiriwa. La saba ni kuwalisha majirani ile akika yake."[3]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) aliulizwa: "Ni ipi sababu hasa ya kichwa cha mtoto kunyolewa?" Akasema: "Kumsafisha dhidi ya nywele za kizazi."[4]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Atakayepata mtoto amwadhinie katika sikio lake la kulia kwa adhana ya Swala, amkimie katika sikio lake la kushoto, hakika hilo ni kinga dhidi ya shetani mlaanifu."[5]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Mtoto anapozaliwa huadhiniwa katika sikio lake la kulia na hukimiwa katika sikio lake la kushoto."[6]

---

[2] *Al-Kafiy* cha Shaikh Kulayniy Juz. 3 Uk. 40, Mlango wa aina za majosho, Hadithi ya 2.
[3] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya saba Uk. 228.
[4] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21 Uk. 424, Mlango wa 44, Hadithi ya 19.
[5] *Al-Kafiy* cha Shaikh Kulayniy Juz. 6 Uk. 24, Mlango wa anayofanyiwa mtoto ambapo ni pamoja na kumwonjesha, Hadithi ya 6.
[6] *Biharul-An'war* Juz. 101 Uk. 122, Mlango wa kupelekwa Sunna, Hadithi ya 60.

# CHAKULA CHA MJAMZITO ALIYESHIKWA NA UCHUNGU

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Chakula cha kwanza cha mjamzito aliyeshikwa na uchungu kiwe ni tende, kwani hakika Mwenyezi Mungu alimwambia Mariam: **"Na litikise kwako shina la mtende, litakudondoshea tende nzuri, zilizoiva." (Sura Maryam: 25)**. Wakasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Iwapo si msimu wa tende?" Akasema: "Tende saba kavu miongoni mwa tende kavu za mji wa Madina, kama hatopata basi ni tende saba kavu miongoni mwa tende kavu za miji yenu, kwani hakika Mwenyezi Mungu amesema: 'Naapa kwa nguvu Yangu, utukufu Wangu, heshima Yangu, na nafasi Yangu ya juu, mjamzito aliyeshikwa na uchungu hali tende siku ya kujifungua na akawa mtoto ni wa kiume ila lazima atakuwa mpole, na akiwa ni wa kike atakuwa mpole pia.'"[7]

# KUMWONJESHA[8] (*TAHNIIK*) NA KUMPA JINA

Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) amesema: "Mmoja wenu akipata mtoto…. Na amwonjeshe maji ya Mto Furati…."[9]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Waonjesheni wanenu tende kavu, hivyo ndivyo alivyowafanyia Mtukufu Mtume Hasan na Husain."[10]

---

[7] *Al-Kafiy* cha Shaikh Kulayniy Juz. 6 Uk. 22, Mlango wa yaliyo Sunna kwa mjamzito na aliyeshikwa na uchungu kula, Hadithi ya 4.

[8] Makusudio ya kumwonjesha hapa ni kabla ya kuanza kunyonya, kwa maana kwamba mtoto akizaliwa kabla ya chakula chochote kuingia kinywani mwake aonjeshwe hayo yaliyoelezwa. – **Mtarjumu**.

[9] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya saba Uk. 228.

[10] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya saba Uk. 229.

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Waonjesheni wanenu maji ya Mto Furati, na udongo wa kaburi la Husain, na kama haiwezekani basi ni maji ya mawinguni (mvua)."[11]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Waonjesheni wanenu udongo wa Husain, kwani hakika wenyewe ni kinga."[12]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Yeyote atakayeonjeshwa maji ya Mto Furati lazima atatupenda Ahlul-Baiti (a.s.)."[13] Na katika Hadithi nyingine: "Ni lazima atakuwa mfuasi wetu."[14]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Ama wakazi wa Mji wa Kufa lau wangewaonjesha watoto wao maji ya Mto Furati wangekuwa wafuasi wetu."[15]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Atakayebahatika kupata watoto wanne wa kiume, na asimpe mmoja wao jina langu bila shaka ameninyanyapaa."[16]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Jiiteni majina mazuri, kwani hakika nyinyi mtaitwa kwayo siku ya Kiyama."[17]

Imepokewa kwamba mtu mmoja alimuuliza Imam Jafar as-Sadiq (a.s.): "Hakika sisi tunawapa majina yenu na majina ya baba zenu, je hilo linatunufaisha?" Imam (a.s.) akasema: "Ndio wallahi."[18]

---

[11] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 407, Mlango wa 36, Hadithi ya 3.

[12] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 115, Mlango wa kupelekwa Sunna, Hadithi ya 35.

[13] *Kaamiluz-Ziyarati* cha Ibn Quwalawihi Uk. 49, Mlango wa 13, Hadithi ya 13.

[14] *Kaamiluz-Ziyarati* cha Ibn Quwalawihi Uk. 49, Mlango wa 13, Hadithi ya 11.

[15] *Safinatul-Bihari* cha Shaikh Abbas Al-Qummiy Juz. 2, Uk. 352.

[16] *Al-Kafiy* cha Shaikh Kulayniy Juz. 6, Uk. 19, Mlango wa majina na kuniya, Hadithi ya 6.

[17] *Al-Kafiy* cha Shaikh Kulayniy Juz. 6, Uk. 19, Mlango wa majina na kuniya, Hadithi ya 10.

[18] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 130, Mlango wa majina na kuniya, Hadithi ya 19.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Hakika zawadi ya kwanza inayopasa mmoja wenu kumpa mwanae ni jina zuri, hivyo mtu atoe jina zuri kwa mwanae."[19]

Imam Ali Al-Hadi (a.s.) amesema: "Ufakiri hautoingia nyumba ambayo humo mna jina: Muhammadi, au Ahmadi au Ali au Hasani au Husaini au Jafar au Talib au Abdullah, au Fatima katika wanawake."[20]

Imepokewa kwamba Imam al-Baqir (a.s.) alimwambia mtoto mdogo: "Jina lako nani?" Akajibu: "Muhammadi." Akasema (a.s.): "Ni ipi kuniya yako?" Akajibu: "Ali." Akasema (a.s.): "Hakika umejiwekea ngome imara dhidi ya shetani. Hakika shetani asikiapo mwenye kuita anaita: 'Ewe Muhammadi! Au ewe Ali!' huyayuka kama yayayukavyo madini ya risasi, hata akisikia muitaji anaita jina la adui miongoni mwa maadui wetu,[21] hutetemeka na kujificha."[22]

Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) amesema: "Majina yasemayo kweli ni yale yaanzayo na Abdu[23] (mja), na yaliyo bora kati ya hayo ni majina ya Manabii."[24]

## AKIKA

**Akika:** Ni dhabihu – itokanayo na mbuzi au kondoo au ngombe au ngamia – ambayo huchinjwa baada ya mtoto kuzaliwa, nayo ni mustahabu kisheria. Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwachinjia akika wanae wawili Hasan na Husain kwa kuchinja kondoo wawili siku ya

[19] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 130, Mlango wa majina na kuniya, Hadithi ya 20.
[20] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 131, Mlango wa majina na kuniya, Hadithi ya 25.
[21] Yaani iwapo huyo adui wa Ahlul-Baiti (a.s.) jina lake ni Ali au Muhammad. – **Mtarjumi.**
[22] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 131, Mlango wa majina na kuniya, Hadithi ya 26.
[23] Mfano: Abdullah, Abdurazaq, Abdul-Ahadi, Abdul-Wahid, Abdurahiim, na mengineyo.
[24] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 129, Mlango wa majina na kuniya, Hadithi ya 17, nukuu kutoka kitabu *Maanil-Akhbar* cha Shaikh Saduq Uk. 146.

saba tangu kuzaliwa kwao.[25] Akika huzingatiwa kuwa ni sadaka kwa ajili ya mtoto na ni kinga ya uhai wake.

Imam Musa Al-Kadhim (a.s.) amesema: "Akika ni wajibu mtu apatapo mtoto…."[26]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Kila mtoto azaliwaye ni rahani kwa Akika."[27]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Akika ni aliye tajiri na kwa fakiri iwapo itamwia wepesi kufanya hivyo, na kama hawezi si juu yake chochote…..na kila mtoto azaliwaye ni rahani kwa Akika yake."[28]

Taabiri ipendezayo kiasi gani!!! Na ubainifu mzuri kiasi gani!!! Hakika Mwenyezi Mungu atakapowazawadia wazazi wawili mtoto anaweza mtoto akaendelea kuishi au Mwenyezi Mungu anaweza kuichukua hiba yake na hivyo mtoto akafariki muda mfupi tu, hivyo atakapochinjiwa Akika bila shaka ataishi (kwa muda mrefu), kwa sababu Akika ni sawa na rahani. Wala hiyo haipingani na hali ya Mwenyezi Mungu kuwa ndiye muhifadhi na mlinzi wa mtoto huyu, na Akika kuwa na athari nyingine za kimazingira ambazo zimewekwa na Mwenyezi Mungu.

## KUINGIA SUNNA

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Waingizeni Sunna wanenu siku saba za mwanzo, hakika kufanya hivyo ni usafi mno na ni tohara kubwa…."[29]

---

[25] *Faraidus-Samtwayn* cha Hamuwini Mshafi Juz. 2, Uk. 104 – 105, chapa ya Lebanon 1400 A.H.

[26] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya saba Uk. 226.

[27] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 120, Mlango wa kuingia Sunna, Hadithi ya 52.

[28] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 121, Mlango wa kuingia Sunna, Hadithi ya 55.

[29] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 108, Mlango wa kuingia Sunna, Hadithi ya 4.

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Waingizeni Sunna wanenu siku ya saba, msizuiliwe na joto wala baridi, hakika kufanya hivyo ni tohara ya mwili, na hakika ardhi hulia kwa kumlalamikia Mwenyezi Mungu kutokana na mkojo wa mwenye govi."[30]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Waingizeni Sunna wanenu siku saba za mwanzo, hakika kufanya hivyo ni tohara kubwa na huharakisha kuota kwa nyama."[31]

## KUNYONYA

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Waepusheni wanenu na maziwa ya malaya na majununi, kwani hakika maziwa huambukiza."[32]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Wachagulieni kwa ajili ya kunyonya kama mnavyochagua kwa ajili ya kuoa, kwani hakika maziwa hugeuza tabia."[33]

## KUWABUSU WATOTO, KUWAKIRIMU NA KUWALEA

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Wabusuni wanenu, kwani kwa kila busu moja mna daraja moja Peponi."[34]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akamtazama mtu mmoja mwenye watoto wawili, kambusu mmoja na kumwacha mwingine, Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Ungefanya usawa baina yao."[35]

---

[30] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 424, Mlango wa 44, Hadithi ya 20.

[31] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nane Uk. 230.

[32] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 20, Uk. 15, Mlango wa 1, Hadithi ya 6.

[33] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 468, Mlango wa 78, Hadithi ya 6.

[34] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya sita Uk. 220.

[35] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya sita Uk. 220.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Fanyeni uadilifu baina ya wanenu kama mpendavyo kufanyiwa uadilifu katika wema na zawadi.”[36]

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Wapendeni watoto wadogo na wahurumieni, na mnapowaahidi kitu watekelezeeni, kwani hakika wao wanawaona nyinyi kuwa ndio mnaowaruzuku.”[37]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Mtoto mwema ni ua zuri miongoni mwa maua ya Peponi.”[38]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Miongoni mwa wema wa mtu ni mtoto mwema.”[39]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Atakayeingia sokoni akanunua tunda na kuwapelekea familia yake, huwa kama aliyebeba sadaka kuwapelekea kaumu wenye haja, na aanze kuwapa watoto wa kike kabla ya wakiume…”[40]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Wakirimuni wanenu na ziboresheni adabu zao mtaghufuriwa.”[41]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Mmoja wenu kumfunza adabu mwanae ni bora kwake kuliko kutoa sadaka pishi moja kila siku.”[42]

---

[36] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya sita Uk. 220.

[37] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 483, Mlango wa 88, Hadithi ya 3.

[38] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya sita Uk. 218.

[39] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 359, Mlango wa 2, Hadithi ya 3.

[40] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya sita Uk. 221.

[41] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 476, Mlango wa 83, Hadithi ya 9.

[42] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya sita Uk. 222.

## SILIKA YA KUJIPENDA

Hakika miongoni mwa mambo ya ndani ambayo Mwenyezi Mungu ameyaweka katika nafsi ya mwanadamu ni silika ya kujipenda, hivyo kila mwanadamu hujipenda mwenyewe kabla ya kila kitu na kabla ya kila mtu. Na hii ni miongoni mwa hekima za juu za Mwenyezi Mungu zilizopo katika viumbe wake na huruma yake kwa waja wake, kwani bila silika hii mwanadamu asingechuma tabia njema wala asingejiepusha na tabia mbaya.

Silika hii inazingatiwa kuwa ni miongoni mwa nguvu zilizomo ndani ya nafsi ya mtoto, na anaweza kuzitumia na kunufaika nazo kwa namna nzuri zaidi iwapo tu atampata mlezi mjuzi na mwalimu wa adabu mwenye uwezo. Na tunaweza kuizingatia silika hii kuwa ni chimbuko la wema wa mtoto iwapo itawezekana kuielekeza katika yaliyo mazuri zaidi. Na wakati huohuo silika hii inaweza kuwa sababu ya msingi ya uovu na adhabu duniani na akhera.

Miongoni mwa njia na mifumo ambayo tunaweza kwayo kuiridhisha na kuituliza silika hii ni kumuheshimu mtoto na kumkirimu na kujali utu wake na mwili wake, kwani mtoto ambaye anaonja utamu wa upole na ukarimu nyumbani kwao, huwa mwanadamu aliye sawa, mwenye roho ya kawaida isiyo kinyume wala isiyokwenda kando, ambayo inatarajiwa kutoa kila kheri na kila jema.

Na kinyume chake ni kwamba lau mtoto akikosa kuheshimiwa na kukirimiwa nyumbani au katika jamii au shuleni, na akawa haonji ila uchungu, ukali, ususuavu wa moyo na dharau, basi dharau itajikita ndani ya nafsi yake na moyo wake hautakuwa na ari, na roho yake itakuwa ni yenye kuumia na yenye huzuni, na athari hizi za kisaikolojia zitadhihiri kupitia matendo yake na kauli zake.

Na mtoto atakuwa ni mwenye kutishiwa na kila upotovu na mwenye kupatwa na kila utelezi, hivyo ataidumbukiza nafsi yake katika dimbwi la hatari na maangamizi, na huko ndiko atakakojuta na hivyo ndivyo jamii itakavyoharibika na kutoweka uwiano wa mtu mmoja mmoja na ule wa kijamii, yatatoweka maadili mema na kuenea utovu wa tabia na uchafu wa kijinsia katika jamii.

Hivyo jamii ni mjumuiko utokanao na mtu mmoja mmoja, nayo inashabihiana na jengo, na watu wanashabihiana na vifaa vya ujenzi ambavyo vimekusanyika na kutengeneza jamii, hivyo kutengemea kwa jamii kunategemea utengemeo wa mtu mmoja mmoja, na kuharibika kwake kunategemea kuharibika kwa mtu mmoja mmoja.

## MFUMO WA MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.) KATIKA KUTENGENEZA JAMII

Alipokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) katika ile jamii iliyoharibika kwa kila aina ya uharibifu wa kijahiliya, iliyochelewa msafara wa kibinadamu na wa kimaendeleo, iliyomong'nyoka pande zake zote na nyanja zake zote, aliazimia (s.a.w.w.) kuitengeneza jamii hiyo kwa njia ya kumtengeneza mtu mmoja mmoja, kwa sababu utengemao huenea kama uharibifu ulivyoenea, na uongofu husambaa kama upotovu unavyosambaa.

Miongoni mwa njia, nyenzo na mbinu ambazo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alizichukua na kuziteua ni kutokomeza chuki za kinafsi ambazo zilijengeka katika nafsi hizo kutokana na athari za kijahilia zilizo ovu. Na kwa kuwa watoto wa leo ndio wakubwa wa kesho, na kwamba miaka ya utotoni ndio mwanzo wa maisha ya mwanadamu, na kwamba silika huamka kwa mtoto na kukua kama akuavyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)

aliweka misingi na kanuni za malezi ya watoto, na akaliweka jukumu hilo juu ya akina baba ambao walisilimu mikononi mwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na wakakubali kutoka kwake amri zake na mafunzo yake kwa kila upokezi na ufuataji, kwa sababu wao walipomwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) waliamini kauli zake zote na amri zake, na hawakuwa na kichocheo chochote kinachowasukuma kutaka kujua sababu na hekma ya mafunzo hayo.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) hakutosheka tu na kutoa mafunzo kuhusu watoto na malezi yao, bali wakati huo huo alikuwa akitengeneza kila alichokiona kimeharibika miongoni mwa hali za watu ambao malezi yao yalikuwa mabaya tangu utotoni, na wakakosa maadili mema kutokana na chuki za kinafsi walizonazo. Hivyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa akiwaheshimu watu na huenda akamtandikia joho lake yule anayeingia kwake, na kunyanyuka sehemu yake kumpisha yule anayeketi kwake japokuwa sehemu ya kuketi ni pana.

Alikuwa akiwatolea salamu watoto na iwapo atapewa mkono na mmoja kati ya Sahaba zake basi Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) huuacha mkono wake mkononi mwake na wala hauondoi toka mkononi mwake mpaka mtu yule auondoe yeye mkono wake toka mkononi mwa Mtume (s.a.w.w.).

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa anagawa mtazamo wake baina ya Sahaba zake, anamtazama huyu na yule kwa usawa, wala hamwachi mtu atembee pamoja naye kwa mguu na hali yeye (s.a.w.w.) yuko juu ya kipando, na alikuwa anawazindua watu na makosa yao, na kuwaongoza kwenye tabia njema na kuwakataza kila kinachoondoa heshima, ubinadamu na dini, na akiwakemea kutenda maovu.

Alikuwa akiwaamuru waheshimiane wao kwa wao, na wawe ndugu wenye kupendana, anawakataza kudharauliana na kudhalilishana, matusi, laana, utesi na mfano wa hayo miongoni mwa maadili machafu. Hivyo akafanikiwa (s.a.w.w.) kuwatengeneza wale waliowezekana miongoni mwa watu wa jamii ile, na hasa kwa njia ya kutengeneza misingi ya malezi inayohusu watoto.

Hakika hali ya kihulka na sifa za kinafsi zilizopo kwa mwanadamu huzingatiwa kuwa ni matokeo ya kimalezi aliyoyapata utotoni toka kwa wazazi wake, hivyo yote aliyojifunza toka kwao kipindi cha utoto, kuanzia mazuri hadi mabaya, huonekana kwake siku za ukubwani.

Kwa ibara nyingine ni kwamba: Mielekeo ya mwanadamu upande wa roho na hulka ni matokeo ya mizizi ya kimalezi iliyopandwa kwake utotoni mwake. Kutokana na dhana hii ni kwamba tukitaka kuujua mustakabali wa wakubwa wa kesho upande wa unyofu au upotovu, usafi au uchafu, nguvu au udhaifu, tunaweza kulijua hilo kupitia njia ya kufuatilia hali za watoto wa leo upande wa malezi na mienendo.

Hivyo nguvu ya utu, utukufu wa nafsi na heshima yake, au mdidimio, uduni wa nafsi na udhaifu wake vilivyopo kwa mwanadamu, hakika ni miongoni mwa mambo ambayo yamejiasisi humo toka kwenye malezi ya wazazi. Hivyo ni wajibu juu ya akina baba na akina mama ambao wanataka kujenga na kutengeneza utu katika nafsi za watoto wao, watilie umuhimu maudhui hii na dhana hizi tangu utotoni mwa watoto wao na tangu udogo wao.

Hakika mtoto anayelelewa katika nyumba yenye dharau, na wazazi wake wanaamiliana naye kama vile yeye si mwanadamu, na wala hajioni kuwa yeye ni kiungo chenye kuheshimika miongoni mwa viungo vya jamii, mtoto kama huyu haitarajiwi awe na utu

ulio sawa, kwa sababu amejijua kuwa yeye ni kiumbe asiyefaa na kwamba ni muovu maishani, kwa sababu amelelewa katika hali ya kudharauliwa, hivyo ni vigumu sifa hii kubadilika kwake.

Hakika wepesi wa malezi sahihi na kukuza sifa njema kwa mtoto hupatikana katika mfumo wa kielimu na wa kimatendo ambao wazazi wana elimu nao, na wanamfuatilia mtoto huyo ili kutekeleza mfumo huo ndani ya nafsi yake. Nyumba ambazo hazijui au zinapuuzia jukumu la malezi ya mtoto, matokeo yake huwa ni kufeli na kutokufanikiwa.

Haifichiki kwamba kuvunja heshima ya mtoto na kumdharau hakufungiki katika namna maalumu au njia maalumu ya udhalilishaji, bali kama ambavyo heshima inaweza kupatikana kwa kauli na kitendo, kadhalika dharau inaweza kupatikana kwa kauli na kitendo.

Hakika nukta ya kwanza katika mfumo wa kanuni kuu za malezi sahihi ni akina baba na akina mama wajue kwamba mtoto ambaye anaishi pamoja nao si mnyama kama kuku na mbuzi, ambaye haja yake inakomea kwenye maji na chakula tu, bali ni wajibu kwao watambue kwamba mtoto ndiye binadamu, lakini yeye ni mdogo aliye dhaifu, na kwamba yeye ni mfano halisi miongoni mwa mifano ya binadamu, na kwamba ana vipaji, uwezo na nguvu vinavyodhihiri nje hatua kwa hatua, na kuimarika toka hatua ya uwezo na kwenda hatua ya kitendo, hivyo kila mwanadamu ni mwandishi kwa uwezo, maana yake anaweza kuandika kwa uwezo wake, akili yake na kipaji chake, hivyo anapojifunza kuandika hapo huwa mwandishi kivitendo.

Hakika akina baba na akina mama ambao wanaamiliana na watoto kwa upole na huruma, na kuwapa nafasi ya kuonyesha uwezo wao wa asili wa kimaumbile, na wala hawawaelekei kwa dhihaka, masikhara na dharau, hakika wao wanawaandalia watoto wao

mazingira mazuri ili zipevuke fikra zao, na nafsi zao zipate heshima kabla ya watoto wengine.

Na upande mwingine ni kwamba, hakika akina baba na akina mama ambao wanawafanyia watoto wao udikteta na ukatili na kuwazingira kwa kitisho cha khofu na mtetemeko, hakika vipaji hivyo vya watoto wao hujiuwa, na husita ule mpevuko wao wa akili kama kinavyojizuia kuendelea, kinavyojizima na kinavyosimama kile chombo kilichokuwa kimewashwa. Kwa ajili hiyo mtoto huisi udhaifu wa kiroho na hatimaye fundo la dharau hujengeka ndani ya nafsi yake.

## MWACHE MWANAO ACHEZE MIAKA SABA

Miongoni mwa silika iliyowekwa katika nafsi ya mtoto ni raghba ya kupenda michezo, hivyo mara hukimbiakimbia na mara hurukaruka, na mara nyingine huchezacheza, na hupata raha kutokana na matumizi yake ya vifaa vya michezo na huiridhisha nafsi yake. Hakika vitendo hivi ambavyo mwanzoni huwa tunavizingatia kuwa ni upuuzi na visivyokuwa na faida, ni miongoni mwa nyenzo muhimu katika kuukuza mwili wa mtoto na kuikomaza roho yake.

Hakika michezo hukomaza neva za mtoto na humsaidia kukomaza mifupa yake, na humfanya apate mazoezi ya aina tofauti za maisha. Hakika michezo huzalisha roho ya ugunduzi na kujitegemea katika kazi, na hudhihirisha vipaji vyake nje kivitendo, na upande mwingine ni kwamba michezo huushughulisha muda wa maisha ya mtoto.

Tunazikuta Hadithi tukufu zilizopokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Maimamu watoharifu (a.s.), zimetamka wazi umuhimu wa michezo katika maisha ya mtoto, na zifuatazo ni baadhi tu ya riwaya hizo:

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Mtoto hucheza miaka saba, hujifunza kuandika miaka saba, na hujifunza halali na haramu miaka saba."[43] Pia (a.s.) akasema: "Mwache mwanao acheze miaka saba…."[44]

Pindi mtoto anapochezea udongo, anachimba shimo au chemba au anajenga kuba la udongo, kisha shimo linabomoka na kubomoka kuba, hapo mtoto hufikiria njia ya kutatua na kuzuia ubomokaji huo, na hapo huchukua hatua za lazima za kuweza kuzuia ubomokaji huo, kuanzia hapa anajifunza ugunduzi katika maisha. Hivyo haipasi wazazi kumkabili kwa dhihaka na dharau, na hapa ndipo inapodhihiri Hadithi ya Mtume (s.a.w.w.): "Wakirimuni wanenu…"[45]

Kutokana na msingi huu serikali zilizopevuka kiakili na zenye mwamko hujenga maeneo ya michezo kwa ajili ya watoto na kuyawekea vifaa vya michezo na burudani ili kuendeleza vipaji vya mtoto, kukomaza roho yake na kuijengea nafsi yake ushujaa. Na linalosikitisha sana ni kwamba: Hakika baadhi ya wahenga wetu na wasimamizi wa mambo yetu walipitwa na nukta hizi muhimu, hivyo wakapuuza malezi ya watoto wao na kuwapa hasara ya dini, dunia na akhera. Kwa msingi huu ikapunguka huruma baina ya akina baba na akina mama, na kudhoofika mahusiano ya huruma na upole kati yao, na bado ujahili huu unaendelea kuwazingira akina baba na akina mama mpaka leo hii, japokuwa sisi tuko katika zama za umeme na Urani.

Ni masikitiko makubwa juu ya wanetu masikini ambao wanafikwa na ukatili, dharau, udhalilishwaji na kunyimwa haki zao

[43] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 474, Mlango wa 83, Hadithi ya 1.

[44] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 475, Mlango wa 83, Hadithi ya 4.

[45] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 476, Mlango wa 83, Hadithi ya 9.

tangu utotoni mwao, na wanakuwa katika shakawa ambayo haina maisha ya furaha baada yake.

## MAJUKUMU YA WAZAZI KATIKA MALEZI YA MTOTO

Hakika kujenga utu kwa mtoto ni miongoni mwa majukumu ya kimalezi ya wazazi, na kuendeleza uwezo huu kwa mtoto kunahitaji ratiba iliyonadhimiwa, kiasi kwamba lau ikifanyiwa kazi kwa umakini na uangalifu wa kina huwa na matokeo mazuri. Hakika kitendo cha wazazi wawili kumuheshimu mtoto na kuishi naye vizuri ni miongoni mwa misingi ambayo ina mchango mkubwa katika kupatikana utu kwa mtoto. Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikusanya mafunzo haya adhimu yenye umuhimu mkubwa katika maneno machache na mafupi, akasema: "Wakirimuni wanenu na wafunzeni adabu njema."

Makusudio ya kuwakirimu hapa ni kumuheshimu mtoto na kuishi naye kufuatana na misingi na kanuni za ubinadamu, hivyo mlezi hana budi kufuata mafunzo haya yenye thamani, na ni lazima juu ya akina baba na akina mama kuwaheshimu watoto wao na wawalindie heshima yao na waamiliane nao muamala mwema, wajiepushe na dharau, kuwapuuza, ukatili na udhalilishaji, ili waweze kulea kizazi chema chenye utu na ubinadamu.

## YAFUATAYO NI BAADHI YA MAFUNZO YA KIMALEZI:

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Wanetu ni maini yetu, wadogo kati yao ni viongozi wetu, na wakubwa kati yao ni

maadui zetu, hivyo wanapoendelea kuishi hutufitini, na wanapofariki hutuhuzunisha."[46]

Akasema tena (s.a.w.w.): "Miongoni mwa haki za mtoto alizonazo kwa mzazi wake ni tatu: Ampe jina zuri, amfunze kuandika na amuoze atakapobalehe."[47]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Waamrisheni wanenu kuswali watakapofikia miaka saba…..watenganisheni vitandani watakapokuwa ni watoto wa miaka kumi."[48]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) anasema: "Mwache mwanao acheze miaka saba na afunzwe adabu miaka saba, na mshirikishe mambo yako miaka saba iwapo amefaulu, la sivyo yeye ni asiye na kheri."[49]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) anasema: "Wanywesheni wanenu Sawiq[50] udogoni mwao, hakika hilo huotesha nyama, na hukomaza mifupa."[51] Na amesema (a.s.): "Atakayekunywa Sawiq siku arubaini mabega yake yatajaa nguvu."[52]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Wafunzeni wanenu kuandika, kwani hakika uandishi ni hima za wafalme na watawala." Akasema tena: "Wafunzeni wanenu kuogelea na shabaha."[53]

---

[46] *Mustadrakul-Wasail* cha Al-Mirza An-Nuriy Juz. 15, Uk. 170, Mlango wa 64, Hadithi ya 3.

[47] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 92, Mlango wa 105, Hadithi ya 19.

[48] *Mustadrakul-Wasail* cha Al-Mirza An-Nuriy Juz. 14, Uk. 188, Mlango wa 99, Hadithi ya 3.

[49] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 473, Mlango wa 82, Hadithi ya 1.

[50] Ni unga ambao hutiwa sukari au maziwa au tende. Kwa ufupi ni chakula kama uji wenye lishe za kisasa zenye mseto wa nafaka mbalimbali. – **Mtarjumi.**

[51] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya kumi na tatu Uk. 192.

[52] *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 306, Mlango wa Sawiq, Hadithi ya 12.

[53] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 21, Uk. 475, Mlango wa 83, Hadithi ya 2.

Imepokewa kutoka kwa Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: "Mtoto atakapofikisha miaka mitatu mwambie: '*Lailaha Ilallah*' mara tatu, kisha huachwa mpaka atimize miaka mitatu na miezi saba na siku ishirini, kisha huambiwa: 'Sema: Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu' mara saba. Huachwa mpaka atimize miaka mine, kisha huambiwa: 'Sema: *Swalatullah Ala Muhammad Waali Muhammad*' mara saba. Kisha huachwa mpaka atimize miaka mitano, kisha huambiwa: 'Ni upi mkono wako wa kulia na ni upi wa kushoto?' Akijua hilo uso wake hugeuziwa kibla na kuambiwa: 'Sujudu.' Kisha huachwa mpaka atimize miaka sita, atakapotimiza miaka sita huambiwa: 'Swali' na hapo hufunzwa rukuu na sijda mpaka atimize miaka saba, akitimiza miaka saba huambiwa: 'Osha uso wako na viganja vyako', atakapoviosha huambiwa: 'Swali', kisha huachwa mpaka atimize miaka tisa, akitimiza hufunzwa udhuu na huchapwa juu ya hilo, na huamuriwa kuswali na huchapwa juu yake, hivyo atakapojifunza udhuu na Swala Mwenyezi Mungu huwaghofiria wazazi wake, inshaallah."[54]

Ewe msomaji laazini! Hivi sasa tayari mtoto amebalehe, amefikia miaka ya ujana ama balehe, na tayari tumetabikisha juu yake sehemu ndogo ya yale yaliyopatikana katika sheria ya Uislamu miongoni mwa adabu, na hivi sasa yupo mwanzoni mwa ujana wake na mpevuko wa umri wake, hivyo ni vizuri ajichagulie kazi na shughuli njema isiyoshusha heshima yake, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu hampendi asiyejishughulisha mwenye kuendekeza kulala. Hebu sasa tuiendee dini ya Uislamu ili tuitambue rai yake kuhusu maudhui hii:

[54] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 94, Mlango wa 105, Hadithi ya 36.

# BIASHARA NA KUTAFUTA RIZIKI YA HALALI

Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammadin (s.a.w.w.) amesema: "Baraka ina sehemu kumi, tisa kati ya hizo zipo katika biashara…."[55]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) anasema: "Hana kheri asiyependa kukusanya mali ya halali, ambayo kwayo atajilinda, atalipia deni lake na ataungia udugu wake."[56]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Kutafuta halali ni faradhi juu ya kila mwislamu wa kiume na wa kike."[57]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa endapo akimtizama mtu na akavutiwa naye husema: "Je ana kazi?" akiambiwa hana, husema: "Hana thamani tena machoni mwangu." Huulizwa: "Vipi hilo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Husema: "Kwa sababu muumini asipokuwa na kazi ataishi kupitia dini yake."[58]

Imamu Zaynul-Abidiina Ali bin Husain (a.s.) amesema: "Miongoni mwa wema wa mtu ni eneo lake la biashara liwe mjini kwake, na wenzi wake wawe watu wema, na awe na kizazi kinachomsaidia."[59]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) anasema: "Mambo matatu ni miongoni mwa wema: Mke mzuri, mtoto mwema, na riziki ambayo kwayo huboresha maisha na kutunza familia yake."[60]

---

[55] *Al-Khiswali* cha Shaikh Swaduq Juz. 2, Uk. 445, Mlango wa 10, Hadithi ya 44.
[56] *Al-Kafiy* Juz. 5, Uk. 72, Mlango wa kuitumia dunia ili kuipata akhera, Hadithi ya 5.
[57] *Biharul-An'war* Juz. 100, Uk. 9, Mlango wa 1, Hadithi ya 35.
[58] *Biharul-An'war* Juz. 100, Uk. 9, Mlango wa 1, Hadithi ya 38.
[59] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 102, Mlango wa 105, Hadithi ya 90.
[60] *Biharul-An'war* Juz. 101, Uk. 103, Mlango wa 105, Hadithi ya 94.

# KUCHAGUA KAZI

Imam Musa al-Kadhim (a.s.) amesema: "Mtu mmoja alikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nimemfunza mwanangu huyu Kitabu hiki,[61] nimpeleke katika kazi gani?' Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akasema: 'Mpeleke kazini wala usimpeleke katika mambo matano: Usimfanye *Sabbu*, wala sonara, wala mchinjaji, wala muuza ngano, wala muuza watumwa.' Akauliza: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! *Sabbu* ni nani?'

"Akasema: 'Yule anayeuza sanda na anatamani vifo vya umma wangu, na mtoto azaliwaye katika umma wangu nampenda sana kuliko vilivyochomozewa na jua. Ama sonara hakika yeye atajishughulisha kuuhadaa umma wangu. Ama mchinjaji yeye atachinja hadi huruma imtoke moyoni mwake. Ama muuza ngano yeye atazuia chakula dhidi ya umma wangu, na mja kukutana na Mwenyezi Mungu na hali ni mwizi ni jambo nilipendalo kuliko akutane Naye na hali ni mwenye kuzuia chakula siku arubaini. Ama muuza watumwa ni kwamba Jibril (a.s.) alinijia na kuniambia: Ewe Muhammad hakika walio shari katika umma wako ni ambao huwauza watu."[62]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Atakaye kuuza na kununua ajiepushe na sifa tano, la sivyo asinunue wala kuuza: Riba, kiapo, kuficha dosari (ya bidhaa), kusifia (bidhaa) atakapoiuza na kushutumu (bidhaa) atakapoinunua."[63]

---

[61] Yaani Qur'ani Tukufu.

[62] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 17, Uk. 137, Mlango wa 21, Hadithi ya 4.

[63] *Al-Kafiy* Juz. 5 Uk. 150, Mlango wa maadili ya biashara, Hadithi ya 2.

Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad (s.a.w.w.) amesema: "Atakayemuhadaa mwislamu katika kununua au kuuza si miongoni mwetu, na atafufuliwa siku ya Kiyama pamoja na Mayahudi, kwa sababu wao ndio viumbe ambao huwahadaa sana waislamu….."[64]

## KILIMO

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Atakayepata maji na udongo kisha akaendelea kuwa fakiri Mwenyezi Mungu humtupilia mbali."[65]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) anasema: "Hakika Mwenyezi Mungu aliwapendelea Manabii wake kazi ya kilimo na ufugaji, ili wasichukie chochote miongoni mwa matone ya mvua."[66]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) aliulizwa kuhusu wakulima, akasema: "Wakulima ndio maghala ya Mwenyezi Mungu aridhini."

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) akasema: "Hakuna kazi ipendwayo sana na Mwenyezi Mungu kuliko kilimo, na Mwenyezi Mungu hakumleta Nabii yeyote ila alikuwa ni mkulima."[67]

---

[64] *Man'layahdhuruhu Al-Faqiihu* Juz. 4, Uk. 14, Mlango wa yaliyokatazwa na Mtume (s.a.w.w.), Hadithi ya 4968.
[65] *Biharul-An'war* Juz. 100, Uk. 65, Mlango wa 10, Hadithi ya 10.
[66] *Biharul-An'war* Juz. 100, Uk. 65, Mlango wa 10, Hadithi ya 8.
[67] *Safinatul-Bihar* Juz. 1, Uk. 549.

# FAMILIA KATIKA UISLAMU

Na sasa kijana anataka kutengeneza na kujenga familia chini ya kivuli cha mafunzo ya Uislamu na si kwa desturi za kuiga na wala si kwa minyororo ambayo watu wamezifungia nafsi zao. Haya hebu sasa ewe kijana twende kwa wale waliobainisha kanuni za kiislamu ili tusikie maneno yao kuhusu ndoa na sifa zake.

Hakika Uislamu unazingatia ndoa kuwa ni kuanzisha uhusiano wa kindoa baina ya mwanaume na mwanamke ili kujenga familia mpya na kupatikana kizazi kipya, na si kuridhisha tu matamanio ya kijinsia tu, wala si kuzituliza hawa za kinyama tu, na wala si kwa ajili ya kumtumikisha mwanamke na kumfanya mtumishi wa mumewe na wanae, bali yeye ni malikia nyumbani kwake na mlezi wa watoto wake.

Hakika shabaha ya ndoa ni kuzaliana na kuongeza kizazi, na kumuhifadhi mwanaume na mwanamke wasiingie katika haramu, hivyo lau watu wangefuata mafunzo ya Uislamu kuhusu maudhui ya ndoa basi isingebaki nafasi ya kuwepo uharibifu, lakini wao wamepuuza kanuni hizo.

Hakika sisi leo hii tunamwona kijana haoi ila baada ya kuhitimu shule baada ya kukamilisha masomo yake ya juu, na baada ya kupata kazi na mshahara unaooana nao, kisha baada ya kupata kazi huenda kuoa akiwa tayari ametimiza kumi la nne la umri wake, wakati ambao ule uzuri wake na mvuto wake vimeshamtoka na hajabakiwa na harakati zake ila chache.

Kisha hakika Uislamu unapendekeza kulisha chakula katika harusi, lakini baadhi ya waislamu wamebadili na kufanya kitendo

cha kulisha chakula ni hafla ya wanandoa au hafla ya ndoa, na hali wanajua fika kwamba gharama za hafla hiyo si chini ya gharama ya kuwalisha chakula jamaa walioalikwa, na kulisha chakula kuna manufaa kwa watu na kunamridhisha mno Mwenyezi Mungu.[68]

Asubuhi ya siku ya kwanza ya fungate maharusi husafiri safari ambayo itatumia muda wa mwezi mzima (fungate ya kitajiri), mwezi huo huitwa mwezi wa asali, safari ambayo humgharimu mume matumizi makubwa japokuwa wao wana haja na mali hiyo siku zijazo, na wanazihitajia kwa ajili ya matumizi mengine ya lazima ya maisha yao, kwa sababu ndio kwanza wako mwanzoni mwa maisha mapya.

Huenda desturi hizi za kuiga, minyororo hiyo na ada hizo ndio zilizopelekea mambo yawe magumu na mazito, na hivyo kuwazuia wengi miongoni mwa vijana kwenda kuoa. Lakini dini ya Uislamu imezitupilia mbali desturi hizi na kufungua hiyo minyororo ambayo imerithisha uovu na adhabu kwa wavulana na wasichana.

Hivyo upande mmoja umeliweka jukumu hili muhimu migongoni mwa wazazi, na ukawaomba wao wawaoze watoto wao wanapobalehe na ukawakataza watu kupindukia katika mahari, hiyo ni ili kusahilisha suala la ndoa na kufunga milango ya madangulo, na

[68] Kisu kimegusa mfupa, kinachosikitisha zaidi ni kuona waislamu wamekuwa ndio vinara wa kunasa katika mtego huu wa Kiyahudi ambao lengo lake ni kuwatenga mbali na mila za Uislamu. Harusi zetu leo Tanzania hazionekani zimefana ila zitanguliwe na rusharoho, mchiriku au matarumbeta, hapo sijakwambia ufirauni na utovu wa maadili unaofanywa katika baadhi ya kichenipati, na baada ya harusi mziki mkubwa wa gharama kubwa hufuatia, na baadae ni sherehe kubwa ya wanandoa. Kinachosikitisha ni kuona jinsi gani baadhi ya familia zinavyojikalifu ili kutekeleza hafla hizi na anasa ambazo mara nyingi zimekuwa zikiandamana na vitendo vya haramu. Mayahudi wamefaulu katika mtego huu ambao Imam Ali (a.s.) alitutahadharisha nao, kwani Imam Ali (a.s.) alisema: “Myahudi akikupa kwa mkono wa kulia atakunyang’anya kwa mkono wa kushoto.” Ndio, mali ambazo wanajamii wangeboreshea maisha yao zinateketea na kuteketezwa katika hafla zisizo na maana kwa kununulia vitu vya anasa ambavyo faida yake huwarudia Mayahudi. – **Mtarjumi.**

hivyo kwenda sawa na mwenendo wa kimaumbile ambao unahitaji kukidhi matamanio ya mwili.

Na hata kama kuwaoza watoto waliobalehe kusingekuwa na faida ila hali ya kujishughulisha kwao na familia na majukumu yake, hilo tu lingetosha, kwani hakika vijana ambao huangukia kwenye mtego wa uhalifu au kujiunga na itikadi batili na kuzitumia nguvu zao katika kuyatumikia makundi hayo maovu, wengi wao ni makapera.

Hakika kijana iwapo angekuwa ni mwenye mke na ana majukumu ya kuitunza familia asingeingia kwenye uharibifu au kwenye makundi hayo ambayo hayawazidishii watu chochote ila hasara, na vipi ataweza kujiingiza humo na hali yeye ni mwenye kushughulishwa na jukumu zito alilo nalo mgongoni?!! Kulihali, hakika katika ndoa kuna masilahi na manufaa ya mtu mmoja mmoja na ya jamii kwa ujumla, kwa wanaume na wanawake, hivyo hebu sasa tukutajie Hadithi kadhaa zilizopatikana kuhusu maudhui hii.

## NDOA

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Muumini asijizuie kuwa na mke, huenda Mwenyezi Mungu atamruzuku kizazi ambacho kitaipa uzito ardhi kwa *Lailaha Ilallah*."[69]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Atakayeoa bila shaka ametimiza nusu ya dini yake, hivyo amche Mwenyezi Mungu katika nusu iliyobaki."[70]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Atakayeacha kuoa kwa kukhofia ufukara bila shaka amemdhania vibaya Mola

[69] *Man'layahdhuruhu Al-Faqiihu* Juz. 3, Uk. 382, Mlango wa ubora wa kuoa, Hadithi ya 4340. *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 20, Uk. 14, Mlango wa 1, Hadithi ya 3.

[70] *Safinatul-Bihar* Juz. 1, Uk. 561.

wake Mlezi, kwa ushuhuda wa kauli Yake: **"Wakiwa mafakiri Mwenyezi Mungu atawatajirisha katika fadhili zake." (Sura Nuru: 32)**"[71]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Ewe kijana oa na jiepushe na zinaa, hakika yenyewe hukung'oa imani moyoni mwako."[72]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Rakaa mbili anazoswali mwenye mke ni bora kuliko Swala ya mtu kapera anayesimama usiku kwa ajili ya ibada na anafunga mchana wake."[73]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Maiti duni kati ya maiti zenu ni za makapera."[74]

Akasema tena (s.a.w.w.): "Wanawake bora katika umma wangu ni wale wenye uso mrembo wenye mahari ndogo."[75]

Akasema (s.a.w.w.): "Aliye tajiri kisha hajaoa huyo si mfuasi wangu."[76]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Je niwaelezeni ni yupi aliye mbora miongoni mwa wanawake wenu? Mwingi wa kizazi, mwingi wa mapenzi na huruma, mkali wa sitara, mtawa, mwenye heshima kubwa katika familia yake, aliye dhalili awapo na mume wake, mwenye kujishaua awapo pamoja na mumewe, mwenye kujihifadhi dhidi ya mwingine, ambaye hufuata kauli yake (mume) na hutii amri yake, na anapokuwa faraghani naye

[71] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya kwanza Uk. 196.
[72] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya kwanza Uk. 196.
[73] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya kwanza Uk. 197.
[74] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya kwanza Uk. 197.
[75] *Man'layahdhuruhu Al-Faqiihu* Juz. 3, Uk. 385, Mlango wa wanawake bora, Hadithi ya 4356.
[76] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya kwanza Uk. 198.

humpa kile anachokitaka (mume) kutoka kwake na wala hatoi kutoa kwa mwanamume."[77]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Tambueni kwamba mwanamke mweusi awapo mwingi wa kizazi ni mtu nimpendaye sana kuliko mzuri asiye na kizazi."[78]

Na akasema (s.a.w.w.): "Mmoja wenu atakapo kuoa aulizie hali ya nywele zake (za mchumba), kama auliziavyo uso wake, kwani hakika nywele ni moja ya uzuri."[79]

Na akasema tena (s.a.w.w.): "Mkeka uliotupwa pembezoni mwa nyumba ni bora kuliko mwanamke asiyezaa."[80]

Na alisema (s.a.w.w.): "Nuksi ipo katika mambo matatu: Katika mnyama, mwanamke na nyumba. Ama mwanamke nuksi yake ni mahari yake kuwa ghali….."[81]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Msiweke ughali katika mahari za wanawake hatimaye zikaja kugeuka uadui."[82]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) anasema: "Atakayeoa na hali mwezi upo katika nyota ya ng'e hatoona uzuri."[83]

---

[77] Yaani haingii moja kwa moja kwenye tendo la kujamiiana bali yeye huonyesha alama fulani ambazo kiakili huonyesha kwamba ana hamu ya tendo la ndoa na yuko tayari kufanya tendo hilo. Jambo ambalo humvutia mno mume na kuleta chachandu halisi katika tendo hilo. – **Mtarjumu**. *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya pili Uk. 200.

[78] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya pili Uk. 203.

[79] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 20, Uk. 59, Mlango wa 21, Hadithi ya 3.

[80] *Man'layahdhuruhu Al-Faqiihu* Juz. 3, Uk. 552, Mlango wa mambo nadra, Hadithi ya 4899.

[81] *Tahdhiibul-Ahkam* Juz. 7, Uk. 399, Mlango wa kuchagua mke, Hadithi ya 2.

[82] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya kumi Uk. 237.

[83] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 20, Uk. 115, Mlango wa 54, Hadithi ya 3.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: "Jiepusheni kuwaoa *Khudharauduman*." Pakasemwa: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! *Khudharauduman* ni akina nani?" Akasema (s.a.w.w.): "Mwanamke mzuri atokanaye na chimbuko ovu."[84]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Oeni vigori, kwani hakika wao wana vinywa visafi mno…."[85]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema kumwambia Ali (a.s.): "Ewe Ali! Hakika Mwenyezi Mungu ameniamuru nikuoze Fatima, nimekuoza kwa mahari ya gramu mia nne za madini ya fedha iwapo tu umeridhia." Ali akasema: "Nimeridhia." Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akasema: "Mwenyezi Mungu awaunganishe pamoja, azipe wema juhudi zenu, awabariki na atoe kutoka kwenu mengi yaliyo mazuri."[86]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) anasema: "Atakayemuoa mwanamke na hali hajanuwia kumpa mahari yake basi huyo mbele ya Mwenyezi Mungu ni mzinifu."[87]

Ibnu Abu Yaafur alimwambia Imam Jafar as-Sadiq (a.s.): "Mimi nataka kumwoa mwanamke na wazazi wangu wanamtaka mwingine." Imam (a.s.) akasema: "Muoe yule uliyempenda na mwache yule aliyependwa na wazazi wako."[88]

---

[84] *Maanil-Akhbari* cha Shaikh Swaduq, Mlango wa maana ya Khudharauduman, Hadithi 1 Uk. 316.

[85] *Al-Kafiy* Juz. 5, Uk. 334, Mlango wa ubora wa vigori, Hadithi ya 1.

[86] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya tatu Uk. 207.

[87] *Man'layahdhuruhu Al-Faqiihu* Juz. 3, Uk. 398, Mlango wa walii, mashahidi, hotuba na mahari, Hadithi ya 4400.

[88] *Al-Kafiy* Juz. 5, Uk. 401, Mlango wa mtu anamtaka mwanamke na wazazi wake wanamtaka mwingine, Hadithi ya 1.

# ADABU ZA USIKU WA KWANZA WA FUNGATE, NA ZILE ZA KUJAMIIANA

Fungu hili la mafunzo yaliyopatikana kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na Ahlul-Bait wake (a.s.) kuhusu usiku wa kwanza wa fungate na kuhusu kujamiiana, inapasa kuliheshimu kwa ajili ya kuhifadhi kizazi na kwa ajili ya usalama wa mke dhidi ya baadhi ya mapungufu.

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) anasema: "Zipelekeni harusi zenu (biharusi) usiku, na lisheni chakula wakati wa dhuha."[89]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) alisema kuwaambia baadhi ya Sahaba zake: "Ukiletewa mke wako mshike nywele za utosi umwelekeze kibla na useme: 'Ewe Mwenyezi Mungu nimemchukua kwa amana yako, nimehalalisha utupu wake kwa maneno yako, hivyo iwapo utanipa mtoto toka kwake mfanye awe mwenye baraka na aliye sawasawa (kimaumbile) wala usimpe shetani ushiriki wala fungu kwake.'"[90]

Ni Sunna katika siku ya kwanza ya fungate kila mmoja mume na mke kuswali rakaa mbili, na baada ya kumaliza Swala mume aanze kuomba dua, hivyo amuhimidi Mwenyezi Mungu na kumtakia rehema Mtume (s.a.w.w.), kisha aseme: "Ewe Mwenyezi Mungu! Niruzuku upendo wake na mapenzi yake, mridhie kwa ajili yangu na niridhie kwa ajili yake, tuunganishe kwa mjumuiko mzuri na kwa muungano rahisi, kwani hakika Wewe unapenda halali na unachukia haramu."[91]

Mume atakapo kumwingilia mkewe aombe dua hii: "Ewe Mwenyezi Mungu niruzuku mtoto na mfanye mchamungu mwerevu,

[89] *Al-Kafiy* Juz. 5, Uk. 366, Mlango wa sunna ya kuoa usiku, Hadithi ya 2.
[90] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 208.
[91] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 208.

asiyekuwa na ziada wala nuksani katika viungo vyake, na fanya mafikio yake ni kwenye kheri."[92] Na ataje jina la Mwenyezi Mungu wakati wa kuanza kumwingilia."

Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-Khudriy kwamba amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alimuusia Ali bin Abu Talib (a.s.) akamwambia: 'Ewe Ali! Biharusi akiingizwa katika nyumba yako mvue viatu vyake pindi anapoketi, na umwoshe miguu yake, na umwagie maji kuanzia kwenye mlango wa nyumba yako mpaka mwisho wa nyumba yako, hakika wewe ukifanya hivyo Mwenyezi Mungu atakuondolea aina elfu za ufakiri toka katika nyumba yako, na atakuingizia humo aina elfu sabini za utajiri, na aina sabini za baraka. Atakushushia rehema sabini zitakazobubujika juu ya kichwa cha biharusi wako mpaka kila pembe ya nyumba yako ipate baraka zake. Biharusi atasalimika na umajinuni na ukoma, havitompata maadamu bado yumo ndani ya nyumba hiyo. Mzuie biharusi katika wiki yake (ya kwanza) asitumie vitu hivi vine: Asinywe maziwa na siki, asile giligilani na tofaha chachu.'

"Ali (a.s.) akasema: 'Ni kwa ila gani nimzuie asitumie vitu vine hivi?' Akasema (s.a.w.w.): 'Kwa sababu uzazi hugeuka na kuwa ugumba na kuacha kuzaa, mkeka uliyopo pembezoni mwa nyumba ni bora kuliko mwanamke asiyezaa.'

"Ali (a.s.) akasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni ipi habari ya siki hadi nayo akatazwe?' Akasema (s.a.w.w.): 'Akipatwa na hedhi kwa sababu ya msukumo wa siki hatotoharika kiukamilifu milele, na giligilani huamsha hedhi tumboni mwake na humwongezea damu ya uzazi. Tofaha chachu huikata hedhi yake na hivyo hugeuka ugonjwa kwake…."'[93]

---

[92] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 209.
[93] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 209.

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: “Hakika mmoja wenu atamwendea mkewe, naye atamkimbia toka chini yake, na lau (mkewe) atampata Mzenji[94] hakika atamng’ang’ania, hivyo mmoja wenu amwendeapo mkewe kuwe na vitangulizi vya tendo la ndoa kati yao, hakika vyenyewe ndio kilainishi cha mambo.”[95]

Umepokewa wasia muhimu sana kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) unaokusanya faida nyingi, nasi hapa tunautaja kiukamilifu:

“Usimwingilie mkeo mwanzo wa mwezi, katikati yake na mwisho wake, kwani hakika umajununi na ukoma na upungufu wa uwezo wa akili humfika haraka yeye na mwanawe.

“Usimwingilia mkeo baada ya adhuhuri, kwani ikiwa mtapata mtoto katika wakati huo atakuwa kengeza, na shetani hufurahia makengeza kwa mwanadamu.

“Usizungumze wakati wa kujamiiana, kwani ikiwa mtapata mtoto hatosalimika na ububu, na wala mmoja wenu asitazame utupu wa mkewe na yapasa afumbe macho yake wakati wa kujamiiana, kwani akitizama utupu atamrithisha upofu, yaani mtoto.

“Usimwingilie mkeo kwa matamanio ya mke wa mwenzako, kwani hakika mimi nahofia iwapo mtapata mtoto atakuwa shoga, mwenye maumbile ya kike, punguwani.

“Atakayepatwa na janaba kwa kuwa kitandani pamoja na mkewe, asisome Qur’ani, kwani hakika mimi nahofia juu yao usiteremke moto toka mbinguni ukawachoma.

“Usimwingilie mkeo ila una kitambaa na mkeo ana kitambaa, na wala msijifute kwa kitambaa kimoja hatimaye yakaja kutokea

[94] Mtu mwenye asili ya maeneo ya Sudan. Nasema: Huenda makusudio ni Mwafrika. –**Mtarjumu**.

[95] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 212.

matamanio juu ya matamanio, hilo kwa hakika huleta uadui kati yenu, kisha huwapelekea kufarakana na kutalikiana.

"Usimwingilie mkeo wima, kwani hakika hicho ni kitendo cha punda, na iwapo mtapata mtoto atakuwa kikojozi kitandani kama punda akojoavyo kila sehemu.

"Usimwingilie mkeo usiku wa kuamkia Idi ndogo, kwani iwapo mtapata mtoto basi hatokuwa mtoto huyo ila mwingi wa shari.

"Usimwingilie mkeo usiku wa kuamkia Idi kubwa, kwani iwapo mtapata mtoto atakuwa na vidole sita au vine.

"Usimwingilie mkeo chini ya mti wenye matunda, kwani iwapo mtapata mtoto atakuwa mjalidi au muuwaji au jasusi muovu.

"Usimwingilie mkeo usawa wa jua na mionzi yake, ila utakapoweka sitara itakayowakinga, kwani hakika iwapo mtapata mtoto ataendelea kuwa katika ukata na ufakiri mpaka atakapofariki.

"Usimwingilie mkeo baina ya adhana na ikama, kwani hakika iwapo mtapata mtoto atakuwa na pupa ya kumwaga damu.

"Mkeo akishika mimba usimwingilie ila upo katika hali ya udhuu, kwani hakika iwapo mtapata mtoto atakuwa kipofu wa moyo na mwenye mkono wa birika.

"Usimwingilie mkeo usiku wa nusu ya Shabani, kwani hakika ikiwa mtapata mtoto atakuwa mlemavu mwenye madoa kwenye nywele zake na usoni kwake.

"Usimwingilie mkeo mwisho wa mwezi iwapo zimebaki siku mbili umalizike, kwani iwapo mtapata mtoto, atakuwa mkusanya kodi za Jamkariyya au msaidizi wa dhalimu, na kundi la watu litahiliki mikononi mwake.

“Usimwingilie mkeo juu ya paa za majengo, kwani hakika iwapo mtapata mtoto atakuwa mnafiki mwenye kujionyesha tena mtu wa bidaa.

“Utakapotoka safarini usimwingilie mkeo usiku huo, kwani hakika mkipata mtoto atatumia mali zake pasipo hakli, – hapo Mtume akasoma: **“Hakika wabadhirifu ni ndugu wa shetani.” (Sura Israi: 27)**

“Usimwingilie mkeo utokapo kwenda safarini safari ya mwendo wa kutwa tatu na usiku wake, kwani hakika mkipata mtoto atakuwa msaidizi wa kila dhalimu.

“Jamiiana usiku wa Jumatatu, kwani iwapo mtapata mtoto atakuwa muhifadhi wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu, mwenye kuridhia yale aliyogaiwa na Mwenyezi Mungu.

“Ukimwingilia mkeo usiku wa Jumanne na mkapata mtoto ataruzukiwa shahada baada ya shahada ya *Lailaha Ilallah Waanna Muhammad Rasululllah*, wala Mwenyezi Mungu hatomwadhibu pamoja na mushrikina, na atakuwa na kinywa chenye harufu nzuri, mwenye moyo wa huruma, mkarimu, mwenye ulimi safi uliosalimika na utesi, uongo na uzushi.

“Ukimwingilia mkeo usiku wa Alhamisi na mkapata mtoto atakuwa hakimu miongoni mwa mahakimu au aalimu miongoni mwa maulamaa.

“Na ukimwingilia mkeo mchana wa Alhamisi wakati jua linakengeuka toka katikati ya mbingu, na ikawa mmepata mtoto, hakika shetani hatomkaribia mpaka azeeke na atakuwa mwelewa na Mwenyezi Mungu atamruzuku usalama wa dini na dunia.

“Na ukimwingilia usiku wa kuamkia Ijumaa na mkapata mtoto bila shaka atakuwa khatibu hodari. Na ukimwingilia mchana

wa Ijumaa baada ya alasiri na mkapata mtoto bila shaka atakuwa maarufu mashuhuri na aalimu.

"Na ukimwingilia usiku wa Ijumaa baada ya nusu ya pili ya usiku bila shaka inatarajiwa utapata mtoto atakayekuwa miongoni mwa watu wema inshaallah.

"Usimwingilie mkeo saa ya mwanzo ya usiku, kwani ikiwa mtapata mtoto hatoacha kuwa mchawi mwenye kuipa dunia kipaumbele kabla ya akhera. Hifadhi wasia wangu huu kama nilivyouhifadhi kutoka kwa Jibril."[96]

Imepokewa kutoka kwa Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: "Usijamiiane mwanzoni mwa mwezi wala katikati yake wala mwishoni, kwani hakika atakayefanya hivyo ajiandae mtoto kuporomoka, na akitimia atakuwa majununi, hivi huoni kwamba majununi wengi hupatwa na umajununi mwanzoni mwa mwezi, katikati yake na mwishoni mwake."[97]

Amesema pia (a.s.): "Usijamiiane ndani ya meli (jahazi, mtumbwi) wala na hali umeelekea kibla au umeipa mgongo."[98]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Atakayemwingilia mkewe na hali yeye ana hedhi kisha mtoto akazaliwa na ukoma na mabalango asimlaumu yeyote ajilaumu mwenyewe."[99]

Mtu mmoja alimwambia Imam Muhammad al-Baqir (a.s.): "Hivi ni karaha kujamiiana baadhi ya nyakati ikiwa ni kwa halali?" Akajibu: "Ndio, kuanzia kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuchomoza kwa jua, na kuanzia kuzama kwa jua mpaka kupotea kwa wekundu

[96] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 209 - 211.
[97] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 212.
[98] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 212.
[99] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 212.

wake, na kutwa ambayo jua limeshikwa, na katika usiku ambao mwezi umeshikwa, na katika mchana na usiku ambao humo kuna upepo mkali mweusi, au mwekundu au wa njano, na mchana na usiku ambao limetokea humo tetemeko…..”[100]

Kundi hili la adabu na mafunzo ya siku ya kwanza ya fungate na ya kujamiiana tumelidondoa na kuliteua kutoka katika vitabu vya Hadithi, na huenda msomaji mwerevu akagundua baadhi ya siri za mafunzo haya na hekima iliyomo ndani ya adabu hizi, ambazo zinaonyesha ni kwa kiwango gani nafsi inaiathiri mimba wakati wa kutunga kwake, na jinsi gani muda, sehemu na mabadiliko yapatikanayo katika anga au ardhi vinavyoiathiri mimba.

## UMILIKI WA ARDHI NA UENDELEZAJI WAKE

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Atakayeendeleza ardhi basi hiyo ni yake.”[101] Hadithi hii ijapokuwa ina umbo dogo na maneno machache ila ni kwamba ina maana nyingi na ni yenye faida nyingi, na lau watawala wangeruhusu na kuidhinisha watu waitabikishe Hadithi hii basi dunia hii ingekuwa nzuri na Pepo iliyojaa neema.

**Maana ya hadithi:** Hakika kila ardhi isiyoendelezwa, yaani isiyo na mazao, miti wala majengo, lau mtu ataiendeleza kwa mfano akachimba humo visima na kutoboa mifereji na mito, akalima miti na mazao mengine, basi kipande hicho cha ardhi kitakuwa chake na ni milki yake, na kitarithiwa na warithi wake baada yake, hiyo ni

[100] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya nne Uk. 213.

[101] *Jawahirul-Kalam* cha Shaikh Muhammad Hasan An-Najafiy Juz. 38, Uk. 7, Kitabu cha kuwahuisha maiti toka ardhini.

sawa ardhi hiyo iwe ukubwa wa mita kumi kwa kumi au farasikhi kumi kwa kumi. Na ni hivyo hivyo lau akiiendeleza kwa jengo na kujenga majumba na makazi.

Tazama lau tungetabikisha katika nchi zetu sheria hii toka katika kanuni za Uislamu, hivi je kuna yeyote angebaki fakiri? Na je tatizo la makazi lingekuwa kubwa kiasi hiki? Na je gharama za kupanga makazi na hoteli zingekuwa kubwa na ghali kiasi hiki? Na je gharama za maisha zingepanda kiasi hiki?

Bali kila mtu angekuwa analima katika ardhi hii pana ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) yale anayoyahitaji miongoni mwa nafaka, matunda na mbogamboga, na angekuwa anatoa hazina za kheri na baraka zilizomo katika tumbo la ardhi hii pana, na angekuwa anafuga katika ardhi yake ndege na wanyama na angenufaika na mazao yake.

Je kungepatikana vijumba vidogo duni visivyokuwa na nafasi na ambavyo havina mwanga wala hewa, isipokuwa hewa nzito na chafu yenye sumu, ambayo inazingatiwa kuwa ni sababu ya msingi ya maradhi na magonjwa katika makazi ya mafakiri na masikini ambao hawana uwezo wa kuyabadili majumba hayo kwa kuyageuza majumba makubwa, na si makasiri marefu, ili walinde afya zao na afya za familia zao na za watoto wao masikini, ambao nyumba haiwatoshi na hivyo wanadharurika kucheza barabarani katika mazingira ya uchafu.[102]

[102] Ukifuatilia maisha ya watu wa hali za kawaida katika Jiji mfano wa Dar es salaam bila shaka utasadikisha maneno ya mwandishi, leo hii nyumba ya vyumba vitano zinaishi humo familia tano, na kila familia si chini ya watu watano, jumla ni watu ishirini na tano, mbaya zaidi nyumba haina jiko wala karo, hivyo chumba hicho hicho ndio varanda ya kufikia wageni, ndio jiko la kupikia, ndio eneo la kulala watu hao watano, hapo bado wageni wasio na taarifa. Hivi kweli maadili yatadhibitiwa? Katika baadhi ya maeneo kama ya Kariakoo katika baadhi ya nyumba chumba kimoja wanaishi zaidi ya watu kumi. Mgeni wangu aliwahi kiniuliza je nyumba hii ya jirani walipatwa na nini jana usiku? Nikamjibu sijui kwa nini umeuliza hilo? Akaniambia: "Nimeamka mapema leo nikaketi hapo nje, watu wazima niliowaona wakitoka katika nyumba hiyo ni zaidi ya

Lau hukmu ya Mwenyezi Mungu ingefuatwa vilivyo katika ardhi!! basi waislamu wasingekuwa na haja ya kuagiza vyakula na riziki kutoka nje, na wala mahakama zisingejaa kesi za wakulima na wamiliki wa ardhi (wala ya wafugaji na wakulima), bali nchi za Uislamu zingekuwa chimbuko la uzalishaji na vituo vya utajiri na watu wangefanikiwa.

## UJENZI WA MAKAZI

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) Amesema: "Miongoni mwa mafanikio ni wasaa wa nyumba."[103] Na akasema tena: "Muumini ana raha katika wasaa wa nyumba."[104]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Hakika nyumba ina heshima na heshima yake ni eneo pana na wenza walio wema, na hakika ina baraka na baraka yake ni uzuri wa eneo lake na upana wa eneo lake na ujirani mwema wa jirani yake."[105]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: "Atakayejenga nyumba achinje kondoo na awalishe nyama yake masikini."[106]

## HAKI ZA JIRANI

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Jibril aliendelea kuniusia kuhusu jirani hadi nikadhani kuwa atarithi."[107] Na akasema

thelathini lakini nyumba yenyewe ndogo, nikadhani huenda walileтewa msiba na hawa wamelala msibani, lakini jinsi wanavyotoka inaniwia vigumu kujiridhisha kwa dhana hiyo." – **Mtarjumi.**

[103] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya tisa Uk. 225.
[104] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya tisa Uk. 225.
[105] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya tisa Uk. 225.
[106] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya tisa Uk. 227.
[107] *Safinatul-Bihar* Juz. 1, Uk. 190.

tena: “Hajaniamini mimi yule ambaye atalala ameshiba na jirani yake ana njaa.”[108]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: “Si miongoni mwetu ambaye haishi vizuri na jirani yake.”[109]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Ambaye anamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho basi asimuudhi jirani yake.”[110]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Hakika Mwenyezi Mungu hapendi watu wa umma wangu kuchungulia kwenye majumba.”[111]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: “Ulizia hali ya jirani kabla ya hali ya wa nyumbani.”[112]

## USAFI

Dini ya Uislamu imeamuru unadhifu na usafi, usafi wa kila kitu, usafi wa mwili, usafi wa kinywa na pua, usafi wa mavazi, usafi wa samani na vyombo. Imewajibisha udhuu na kuoga na ikawajibisha kuswali ndani ya nguo tohara na ikawaamuru watu kujiepusha mbali na uchafu na najisi. Ufuatao ni baadhi ya ufafanuzi wake:

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Usafi ni sehemu ya imani…”[113]

[108] *Safinatul-Bihar* Juz. 1, Uk. 190.
[109] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 668, Mlango wa haki za ujirani, Hadithi ya 11.
[110] *Al-Kafiy* Juz. 5, Uk. 667, Mlango wa haki za ujirani, Hadithi ya 6.
[111] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa kumi na mbili, Sura ya tatu Uk. 435.
[112] *Biharul-An’war* Juz. 73, Uk. 155, Mlango wa 26, Hadithi ya 36.
[113] *Biharul-An’war* Juz. 59, Uk. 291, Mlango wa 26, Hadithi ya 89.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Fagieni maeneo ya nyumba zenu na wala msijishabihishe na Mayahudi."[114]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Kuosha chombo na kufagia maeneo ya nyumba huleta riziki."[115]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Msilaze uchafu ndani ya majumba yenu, kwani hakika wenyewe ni makazi ya shetani."[116]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Nyumba nzuri ni hamamu, humo moto hukumbukwa na uchafu na adha huondolewa."[117] Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikataza kukojoa katika maji yaliyotuwama.[118]

## USAFI WA KINYWA NA PUA

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Mmoja wenu asukutue kinywa na apandishe maji puani, kwani hakika ni ghufurani ya madhambi yenu na humfukuza shetani."[119]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Kusukutua kinywa na kusafisha pua ni Sunna na ni tohara ya kinywa na pua."[120]

---

114 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya tisa Uk. 127.
115 *Al-Khiswal* cha Shaikh Swaduq Juz. 1, Uk. 54, Mlango wa 2, Hadithi ya 73.
116 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa kumi na mbili, Sura ya pili Uk. 425.
117 *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 496, Mlango wa hamamu, Hadithi ya 1.
118 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa kumi na mbili, Sura ya pili Uk. 424.
119 *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 1, Uk. 432, Mlango wa 29, Hadithi ya 11.
120 *Al-Khiswal* cha Shaikh Swaduq Juz. 2, Uk. 611, Hadithi ya 400.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Ewe Ali! Ni juu yako kupiga mswaki kila wakati wa kutawadha."[121]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akasema tena: "Lau si kukhofia kuwasababishia uzito umma wangu ningewaamuru kupiga mswaki kila wakati wa udhu wa kila Swala."[122]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Katika kupiga mswaki kuna sifa kumi na mbili: Ni katika Sunna, ni kisafisho cha kinywa, king'arisho cha macho, humridhisha Rahman, hung'arisha meno, huondoa umanjano juu ya meno, huimarisha fizi, huleta hamu ya kula, hiondoa balghamu, huongeza nguvu ya kuhifadhi vitu, huongeza mema na kuwafurahisha malaika."[123]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Safisheni njia ya Qur'ani." Wakasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni ipi njia ya Qur'ani?" Akasema: "Vinywa vyenu." Wakasema: "Tusafishe kwa kitu gani?" Akasema: "Kwa mswaki."[124]

Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) amesema: "Swala ya rakaa mbili ya mtu aliyepiga mswaki ni bora kuliko ya rakaa sabini ya mtu ambaye hajapiga mswaki."[125]

## KUNYOA NYWELE

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Mmoja wenu asirefushe masharubu yake, hakika shetani atayafanya maficho ya kujifichia."[126]

[121] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 2, Uk. 17, Mlango wa 3, Hadithi ya 2.
[122] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 2, Uk. 17, Mlango wa 3, Hadithi ya 4.
[123] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa pili, Sura ya tatu Uk. 50.
[124] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa pili, Sura ya tatu Uk. 51.
[125] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa pili, Sura ya tatu Uk. 50.
[126] *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 487, Mlango wa ndevu na masharubu, Hadithi ya 11.

Akasema tena: "Miongoni mwa Sunna ni kupunguza masharubu mpaka yafikie usawa wa mdomo wa juu."[127]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Kukata kucha na kupunguza masharubu, toka ijumaa moja mpaka ifuatayo ni kinga ya ukoma."[128]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Ambaye anamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho asiache nywele zake za sehemu ya siri zaidi ya siku arubaini. Wala si halali kwa mwanamke ambaye anamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuziacha mwilini mwake zaidi ya siku ishirini."[129]

Akasema tena: "Mmoja wenu asirefushe nywele za kwapani mwake, kwani hakika shetani atazigeuza maficho ya kujifichia."[130]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Kunyoa nywele za puani hupendezesha uso."[131]

## USAFI WA MAVAZI

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu ni Jamala anapenda jamala, na anapenda kuona kwa waja wake athari za neema yake."[132]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Katika nguo zenu hakuna iliyo nzuri kuliko nyeupe, hivyo ivaeni na wakafinieni maiti zenu."[133]

---

[127] *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 487, Mlango wa ndevu na masharubu, Hadithi ya 6.
[128] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nne, Sura ya kwanza Uk. 64.
[129] *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 506, Mlango wa sehemu za siri, Hadithi ya 11.
[130] *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 507, Mlango wa kwapa, Hadithi ya 1.
[131] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 2, Uk. 118, Mlango wa 68, Hadithi ya 1.
[132] *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 438, Mlango wa kujipendezesha na kuonyesha neema, Hadithi ya 1.
[133] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya tatu Uk. 104.

Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) amesema: "Kuzikunja nguo zenu ndio raha yake, nako huzipelekea kudumu."[134] Pia amesema: "Nguo safi humzuia adui."[135]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Kufua nguo huondoa ghamu na huzuni, na ni tohara ya Swala…"[136]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Atakayepata nguo aisafishe."[137]

## DUA NA VIGAWANYO VYAKE

Mwislamu akisema: "Assalam Alaykum." Huwa amemwombea dua msalimiwa kwa kumuombea usalama dhidi ya kila baya, nayo ni alama ya waislamu na hupandikiza mapenzi na upendo na huondoa nongwa na huzima ghadhabu.

Linalosikitisha sana ni kwamba baadhi ya waislamu katika zama zetu hizi imekuwa vigumu kwao kutoa salamu ya kiislamu, hivyo utawaona wanaishia kuinua mkono badala ya salamu. Na wengine miongoni mwa waislamu wamewaiga manaswara katika salamu, hivyo mmojawapo amwonapo mwenzake huvua kofia kichwani mwake. Na wengine wamebadili salamu kwa kauli: "Asubuhi njema." au "Jioni njema." au "Haloo!!".

Hivi si vibaya na aibu mwislamu aache salamu ya dini yake ambayo Mwenyezi Mungu amemwamuru Nabii wake (s.a.w.w.) kwayo, kisha aige mila za makafiri na mushrikina?!!!

134 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya pili Uk. 103.
135 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya pili Uk. 103.
136 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya pili Uk. 103.
137 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa sita, Sura ya pili Uk. 103.

Salamu ni Sunna iliyosisitizwa, nayo ina manufaa duniani na malipo huko akhera. Yafuatayo ni baadhi ya mafunzo ya kiislamu katika nyanja hii.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Salamu ya mwislamu kwa nduguye mwislamu ni amwombee amani atakapokutana naye…" Pia akasema: "Bakhili mno kati ya watu ni yule anayebania salamu."[138] Pia akasema: "Anzeni salamu kabla ya mazungumzo, hivyo atakayeanza mazungumzo kabla ya salamu msimjibu."[139]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Hakika mimi huwasalimia wanawake, na wala simsalimii msichana miongoni mwao, kwa kuwa mimi nakhofia sauti yake isinivutie, nikaja kupatwa na mengi kuliko yale malipo niliyotafuta."[140]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Hakika muumini atakapokutana na nduguye, kisha akamwambia: 'Jitanafasi.' Ataandikiwa kujitanafasi mpaka Siku ya Kiyama."

Pia akasema: "Mdogo amsalimie mkubwa, mwenye kupita amsalimie aliyeketi, na wachache wawasalimie wengi."[141]

Na akasema tena: "Hakika ukamilifu wa salamu ya kumtolea asiye safarini ni kupeana mikono, na ukamilifu wa salamu ya kumtolea msafiri ni kumkumbatia."[142]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) anasema: "Waumini wawili wakikutana na wakapeana mikono, Mwenyezi Mungu huwageukia kwa uso wake, na huporomoka madhambi toka kwao kama yapukutikavyo majani toka mtini."

---

[138] *Amali* cha Tusiy, Uk. 88, Hadithi ya 136.
[139] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 644, Hadithi ya 3.
[140] *Biharul-An'war* Juz. 101 Uk. 37, Mlango wa 91, Hadithi ya 26.
[141] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 646, Mlango wa ambaye ni lazima kuanza kutoa salamu, Hadithi ya 1.
[142] *Tuhaful-Uquul,* Uk. 360.

## DUA YA HAMAMUNI

Imam Hasan bin Ali (a.s.) alitoka hamamu, ndipo mtu mmoja akamwambia: "Kupendeze kuoga kwako." Imam (a.s.) akamkataza ibara hii, yule mtu akasema: "Nisemeje?" Imam (a.s.) akasema: "Sema: Yapendeze yale yaliyotoharika toka kwako, na yatoharike yale yaliyopendeza toka kwako."[143]

Imam as-Sadiq (a.s.) amesema: "Ndugu yako akikwambia wakati umetoka hamamu: "Hamamu yako ipendeze." Mwambie: "Mwenyezi Mungu akuneemeshe."[144]

## DUA YA MWENYE KUTOA CHAFYA

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Mtu akitoa chafya muombeeni rehema hata kama yupo kisiwani." Na katika riwaya nyingine: "Hata kama yupo nyuma ya bahari."[145]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) anasema: "Mmoja wenu akitoa chafya muombeeni rehema, semeni: 'Mwenyezi Mungu akurehemu.' Naye aseme: 'Mwenyezi Mungu awaghofirie na awarehemuni.' Mwenyezi Mungu amesema: **"Na mnaposalimiwa kwa maamkizi yoyote, basi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au mrejeshe hayo hayo." (Sura Nisai: 86)**."[146]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) anasema: "Huombewa rehema mara tatu yule mwenye kutoa chafya, zaidi ya hapo ni ugonjwa."[147]

[143] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tatu, Sura ya kwanza Uk. 54.
[144] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tatu, Sura ya kwanza Uk. 54.
[145] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 653, Mlango wa kutoa chafya na kuombewa dua, Hadithi ya2.
[146] *Al-Khiswal* Juz. 2, Uk. 633, Hadithi ya mia nne.
[147] *Al-Khiswal* Juz. 1, Uk. 126, Mlango wa tatu, Hadithi ya 124.

Pia akasema: "Mwenye kutoa chafya akitoa zaidi ya mara tatu, huambiwa: 'Mwenyezi Mungu akuponye.' Kwa sababu huo ni ugonjwa."[148]

Daudi bin Haswini amepokea kwamba: "Tulikuwa kwa Abu Abdillah as-Sadiq (a.s.), ndani ya nyumba nilihesabu watu kumi na nne, Abu Abdillah (a.s.) akatoa chafya, na hakuna yeyote aliyeongea, ndipo Abu Abdillah (a.s.) akasema: 'Hivi hamwombi? Wajibu wa muumini juu ya muumini mwenzake ni amtembelee atakapougua ……na amwombee rehema atakapotoa chafya…."[149]

## PONGEZI YA KUPATA MTOTO

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Mtu mmoja alimpongeza mwenzake aliyepata mtoto, akasema: 'Hongera kwa kumpata mpiganaji mpanda farasi.' Hasan bin Ali (a.s.) akamwambia: 'Nani aliyekujuza kwamba ni mpiganaji mpanda farasi au ni mpiganaji mtembea kwa miguu?' Yule mtu akasema: 'Mimi ni fidia kwako, je nisemeje?' Akasema: 'Sema: Mshukuru mpaji na ubarikiwe kwa uliyepewa, afikie utu uzima na uruzukiwe wema wake."'[150]

## KUMKIRIMU MGENI

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Watu wawili waliingia kwa Amirul-Muuminina Ali (a.s.), naye akampa kila mmoja wao mto, mmoja akaukalia mwingine akakataa, Amirul-Muuminina Ali (a.s.) akasema: Ukalie kwani hakika hakatai kukirimiwa ila punda…."[151]

[148] *Al-Khiswal* Juz. 1, Uk. 127, Mlango wa tatu, Hadithi ya 125.
[149] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 654, Mlango wa kutoa chafya na kuombewa dua, Hadithi ya7.
[150] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa nane, Sura ya sita Uk. 221.
[151] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 12, Uk. 101, Mlango wa 69, Hadithi ya 1.

Imam Ridha (a.s.) amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: 'Miongoni mwa haki za mgeni (zilizopo kwako) ni utembee naye, umsindikize toka katika sehemu yako ya heshima hadi mlangoni."[152]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Usimwambie ndugu yako atakapoingia nyumbani kwako: 'Umeshakula leo?' Lakini mkaribishe ulichonacho, kwani hakika ukarimu wote ni kutoa ulichonacho."[153]

## ADABU YA KULA

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Atakayeosha mkono wake kabla ya chakula na baada yake, ataishi kwa wasaa na atapata afya njema kwa mwili wake kukingwa na maradhi."[154] Pia akasema: "Mmoja wenu akiketi kwenye chakula akae mkao wa mtumwa na ale juu ya ardhi…"[155]

Pia alisema: "Katu usivimbewi, hiyo ni kwa sababu mimi sianzi chakula ila husema: 'Bismillahi.' Na huwa simalizi kula ila husema: 'Alhamdulilahi.'"[156]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Ewe Ali! Anza kula chakula chako kwa chumvi na malizia kwayo, yenyewe ina ponyo la maradhi sabini, kati ya hayo ni ukoma na kifafa…."[157]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) alisema: "Nimemdhamini mwenye kusoma Bismillahi juu ya chakula chake kwamba

---

152 *Uyuun Akhbarir-Ridha* Juz. 2, Uk. 75, Mlango wa 31, Hadithi 323.
153 *Safinatul-Bihar* Juz. 2, Uk. 76.
154 *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 290, Mlango wa kuchukua udhu kabla na baada ya kula, Hadithi ya 1.
155 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya tatu Uk. 141.
156 *Biharul-An'war* Juz. 63, Uk. 380, Mlango wa kuomba dua na kuhimidi, Hadithi ya 47.
157 *Biharul-An'war* Juz. 63, Uk. 398, Mlango wa 13, Hadithi ya 20.

hakitomdhuru." Ibnu Al-Kawwa[158] akasema: "Ewe Amirul-Muuminina! Jana usiku nilikula chakula na nilikisomea Bismillahi lakini kilinidhuru." Akasema (a.s.): "Ulikula aina nyingi na ulisomea baadhi yake na hukusomea aina nyingine ewe uliye mwovu."[159]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Usile na hali watembea ila utakapodharurika kufanya hivyo."[160]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) alisema: "Atakayekula chakula katika hali ya usafi, akatafuna vilivyo chakula, akakiacha chakula na hali bado anakitamani, na akawa hajazuia haja kubwa ilipomshika, basi hatougua ila ugonjwa wa kifo chake."[161]

Akasema tena: "Mzee mtu mzima haipasi alale ila na tumbo lake liwe limejaa chakula, kwani hali hiyo humletea usingizi mwanana na husababisha harufu nzuri kinywani mwake."[162]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Yeyote miongoni mwenu akialikwa kwenye chakula asimbebe mwanae, kwani iwapo atambeba atakula haramu na ataingia (eneo la nyumba) na hali ni mwenye kupora."[163]

Akasema tena: "Kula na hali umeshiba huleta upofu."[164] Akasema mahali pengine: "Kula sokoni ni uduni."[165]

---

158 Huyu alikuwa ni miongoni mwa Makhawariji, na mara kwa mara alikuwa akijaribu kutaka kumpinga na kumkosoa Imam Ali (a.s.).

159 *Biharul-An'war* Juz. 63, Uk. 369, Mlango wa kuomba dua na kuhimidi, Hadithi ya 6.

160 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya tatu Uk. 145.

161 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya tatu Uk. 146.

162 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya tatu Uk. 147.

163 *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 270, Mlango wa aliyekwenda kwenye chakula ambacho hajaalikwa, Hadithi ya 1.

164 *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 269, Mlango wa karaha ya kula sana, Hadithi ya 7.

165 *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 24, Uk. 395, Mlango wa karaha ya kula sokoni, Hadithi ya 2.

Imam Ridha (a.s.) amesema: "Unapokula nyoosha mgongo wako na weka mguu wako wa kulia juu ya mguu wa kushoto."[166]

## KUCHOKOA MENO

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Kile ulichokizungushia ulimi wako na hatimaye ukakitoa kimeze. Ama kile ulichokitoa kwa kuchokoa meno kitupe."[167]

Aliulizwa Imam Al-Kadhim (a.s.) kuhusu kiwango cha kuchokoa meno, akasema: "Ni kuondoa kichwa chake (cha baki la chakula) ili asisababishe fizi kutoa damu."[168]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Safisheni vinywa vyenu kwa kuchokoa meno."[169]

Imam Ridha (a.s.) amesema: "Msichokoe meno kwa kutumia kijiti cha mkomamanga, mua wala kwa ufito wa henzerani, kwani hakika hayo huamsha asili ya ukoma, na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa akichokoa kwa kila alichokipata ila mua na mwanzi."[170]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Chokoeni kwa kutoa mabaki ya chakula, kwani kitendo hicho huupa mwili na meno siha, na huleta riziki kwa mja."[171]

---

166 *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 299, Mlango wa vitu nadra, Hadithi ya 21.
167 *Manla'yahdhuruhu Al-Faqiihu* Juz. 3, Uk. 357, Mlango wa adabu za kula na kunywa, Hadithi ya 4262.
168 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya tano Uk. 152.
169 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya tano Uk. 152.
170 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya tano Uk. 152.
171 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya tano Uk. 153.

# ADABU YA KUNYWA MAJI

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Jiepushe kukithirisha kunywa maji kwani hakika hilo ni sababu ya kila ugonjwa."[172]

Amesema tena: "Lau wao wangepunguza kunywa maji miili yao ingeimarika."[173]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Kunyweni maji hatua kwa hatua (kidogo kidogo), wala msinywe maji moja kwa moja bila kuhema, kwani kufanya hivyo husababisha ugonjwa wa ini."[174]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "…..wala mmoja wenu asinywee maji sehemu ya shikio la chombo, kwani hapo ni sehemu ya mkusanyiko wa uchafu."[175]

Pia amesema: "Kunyweni kwa mikono yenu, kwani yenyewe ndio chombo bora kati ya vyombo vyenu."[176]

Imepokewa kutoka kwa Daud ar-Riqiy amesema: "Nilikuwa kwa Abu Abdillah as-Sadiq (a.s.) alipoomba maji ya kunywa, alipoyanywa nilimuona macho yake yamejaa machozi na kwikwi ya kilio ikimtoka, akasema: 'Ewe Daud! Mwenyezi Mungu amlaani aliyemuuwa Husain, hakuna mja atakayekunywa na akamkumbuka Husain na kumlaani muuwaji wake ila Mwenyezi Mungu atamwandikia mema laki moja, na atamfutia madhambi laki moja, na atainuliwa daraja laki moja, na ni kama aliyewapa uhuru watumwa

[172] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya saba Uk. 157.
[173] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa saba, Sura ya saba Uk. 157.
[174] *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 381, Mlango wa fadhila za kunywa maji, Hadithi ya 1.
[175] *Manla'yahdhuruhu Al-Faqiihu* Juz. 4, Uk. 4, Mlango wa yaliyokatazwa na Mtume, Hadithi ya 4968.
[176] *Al-Kafiy* Juz. 6, Uk. 385, Mlango wa vyombo, Hadithi ya 7.

laki moja, na Mwenyezi Mungu atamfufua Siku ya Kiyama na hali ni mwenye kifua baridi.”’[177]

## SAFARI NA ADABU ZAKE

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Safirini mpate afya….”[178]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Safirini kwani ikiwa nyinyi hamtafaidika kwa kupata mali mtafaidika kwa kupata akili.”[179]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Safari ni mizani ya watu.”[180]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Mwenyezi Mungu amewalaani watu wa aina tatu:….na mwenye kusafiri peke yake.”[181]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) alisema: “Ulizia rafiki kabla ya njia….”[182]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: “Anayetaka kusafiri asafiri siku ya jumamosi, lau jiwe lingechomoka toka mlimani siku ya jumamosi, basi Mwenyezi Mungu angelirudisha sehemu yake….”[183]

---

177 *Maaliy Sibtwayni* cha Mazandarani Juz. 1, Uk. 314, Baraza la saba kuhusu kiu ya Ahlul-Baiti (a.s.).
178 *Al-Mahasin* cha Barqiy Juz. 2, Uk. 79.
179 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya kwanza Uk. 240.
180 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya kwanza Uk. 240.
181 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya sita Uk. 259.
182 *Biharul-An'war* Juz. 73 Uk. 229, Mlango wa 48, Hadithi ya 10.
183 *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya kwanza Uk. 240.

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Toa sadaka na usafiri, yaani siku utakayo."[184]

## TABIA NJEMA ZA SAFARINI

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Si katika murua mtu kusimulia kheri au shari iliyompata safarini."[185]

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) alisema: "Usisuhubiane naye safarini yule ambaye hathamini ihsani yako juu yake kama unavyothamini ihsani yake juu yako."[186]

Shihab bin Abdurabih amesema: "Nilimwambia Abu Abdillah as-Sadiq (a.s.): 'Unaijua hali yangu na utajiri wangu na kuwatosheleza kwangu ndugu zangu, je nikisuhubiana na baadhi yao kwenda Makka niwatosheleze?' Akasema (a.s.): 'Usifanye hivyo ewe Shihab, kwani hakika ukitoa nao wakatoa utawapunja, na ikiwa wao wataacha kutoa utawadhalilisha, hivyo suhubiana na watu kifani chako."[187]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Usuhuba mzuri upendwao na Mwenyezi Mungu ni wa watu wane, wakizidi watu saba huwa hakuna ila kelele zao."[188]

Tena akasema (s.a.w.w.): "Kiongozi wa watu ndio mhudumu wao safarini."[189]

---

[184] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya pili Uk. 243.
[185] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya nne Uk. 250.
[186] *Al-Kafiy* Juz. 4, Uk. 286, Mlango wa wasia, Hadithi ya 5.
[187] *Al-Kafiy* Juz. 4, Uk. 287, Mlango wa wasia, Hadithi ya 7.
[188] *Al-Kafiy* Juz. 8, Uk. 303, Mlango wa mustahabu wa kumchukua rafiki safarini, Hadithi ya 464.
[189] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya nne Uk. 251.

Na alisema (s.a.w.w.): “Miongoni mwa heshima ya mtu ni kubeba matumizi mazuri atokapo kwa ajili ya safari.”[190]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Mmoja wenu akienda safarini na akarudi na kuungana na familia yake, awape zawadi, awazawadie angalau jiwe.”[191]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: “Hakika wewe utasuhubiana na watu mbalimbali, hivyo usiwaambie: ‘Teremkeni hapa na msiteremke hapa’, kwani miongoni mwao yumo anayekutosheleza.”[192]

Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) amesema: “Usitembee mwendo mrefu bila kuvaa viatu, wala usiteremke usiku toka juu ya mnyama wako ila nawe miguuni umevaa viatu, wala usikojoe katika mfereji wa maji, wala usionje mbogamboga na wala usiinuse ila baada ya kujua ni ipi, wala usipeleke kiriba mdomoni ili kunywa mpaka ujue ndani kina nini, wala usitembee ila pamoja na yule unayemtambua, jitahadhari na yule usiyemtambua.”[193]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Ni wajibu juu ya mwislamu anapotaka kusafiri awajulishe ndugu zake, na ni wajibu juu ya ndugu zake atakaporejea waende kumwona.”[194]

---

[190] *Al-Kafiy* Juz. 8, Uk. 303, Mlango wa mustahabu wa kumchukua rafiki safarini, Hadithi ya 467.
[191] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya nane Uk. 266.
[192] *Makarimul-Akhlaq* cha Sheikh Tabarasiy, Mlango wa tisa, Sura ya nane Uk. 267.
[193] *Biharul-An'war* Juz. 75, Uk. 189, Mlango wa wasia wa al-Baqir (a.s.), Hadithi ya 46.
[194] *Wasailus-Shia* cha Shaikh Al-Huru Al-Amiliy Juz. 11, Uk. 448, Mlango wa 56, Hadithi ya 1.

## BARUA NA MAWASILIANO

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Mawasiliano ya wanandugu wawapo nyumbani ni kutembeleana, na wawapo safarini ni kuandikiana barua."[195]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Kujibu barua ni wajibu kama ulivyo wajibu wa kujibu salamu."[196]

Imam Jafar as-Sadiq (a.s.) amesema: "Msiache *Bismillahi Rahman Rahiim*, hata kama baada yake litafuata shairi."[197]

## URAFIKI

Rafiki ni yule anayefanya urafiki nawe kwa upendo wake wa dhati na siri yake inaoana na siri yako, kama ambavyo dhahiri yake inavyooana na dhahiri yako, na bila shaka zimepatikana habari na Hadithi nyingi kuhusu maudhui hii, nasi hapa tutataja chache kati ya hizo:

Imam Hasan al-Mujtaba (a.s.) amesema: "…..Na ikiwa haja itakusukuma kufanya urafiki na mtu basi fanya urafiki na yule ambaye lau ukifanya naye urafiki atakupamba, ukimhudumia atakuhifadhi, ukitaka msaada kutoka kwake atakusaidia, ukisema ataisadikisha kauli yako, ukishambuliwa atasaidia shambulizi lako, na ukimfanyia ihsani naye atakufanyia ihsani, ikijitokeza aibu toka kwako huisitiri, akiona jema toka kwako hulithamini, ukimwomba atakupa na ikiwa umenyamaza bila kuomba atakuanza kwa kukupa, ukipatwa na moja ya maafa hukuhuzunikia, ambaye shari yake haikufiki na wala hakusumbui kwa haja za mara kwa mara, na wala hakuangushi katika mipango….."[198]

---

[195] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 670, Mlango wa kuandikiana barua, Hadithi ya 1.
[196] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 670, Mlango wa kuandikiana barua, Hadithi ya 2.
[197] *Wasailus-Shia* Juz. 12, Uk. 136, Mlango wa 94, Hadithi ya 1.
[198] *Biharul-An'war* Juz. 44, Uk. 139 – 140, Mlango wa 22.

Imam as-Sadiq (a.s.) amesema: "Usimpe rafiki yako siri yako ila ile ambayo lau adui yako akiijua hatokudhuru, kwani hakika rafiki siku moja anaweza kugeuka kuwa adui."[199]

Akasema tena: "Jihadhari na adui yako mara moja, na jihadhari na adui yako mara elfu moja. Huenda rafiki akageuka na kuwa adui na hivyo akajua vizuri namna ya kukudhuru."

Imam as-Sadiq (a.s.) amesema: "Akupendaye zaidi miongoni mwa ndugu ni yule akuonyeshaye mapungufu yako kwa kukupa nasaha, na si yule akufichiaye mapungufu yako kwa kukuhadaa."

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: "Mtu hutambulika kupitia mwenzake."

## TABIA NJEMA

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Hakika mwenye tabia njema ana ujira mfano wa mtu mwenye funga mwenye kusimama usiku kwa ajili ya ibada."[200]

Akasema tena: "Siku ya Kiyama hakuna kitu bora kitakachowekwa katika mizani ya mtu kuliko tabia njema."[201]

Akasema (s.a.w.w.): "Ni juu yenu kuwa na tabia njema, hakika mwenye tabia njema hana kipingamizi na pepo. Na jiepusheni na tabia mbaya, kwani hakika mwenye tabia mbaya hana kipingamizi na moto."[202]

Akasema tena: "Tabia mbaya huharibu amali kama siki inavyoharibu asali."[203]

[199] *Biharul-An'war* Juz. 72, Uk. 71, Mlango wa 45, Hadithi ya 12.
[200] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 100, Mlango wa 104, Hadithi ya 5.
[201] *Al-Kafiy* Juz. 2, Uk. 99, Mlango wa 104, Hadithi ya 2.
[202] *Wasailus-Shia* Juz. 12, Uk. 152, Mlango wa 104, Hadithi ya 17.
[203] *Wasailus-Shia* Juz. 12, Uk. 152, Mlango wa 104, Hadithi ya 18.

Akasema (s.a.w.w.): “Atakayeketi karibu nami Siku ya Kiyama ni yule mwenye tabia njema miongoni mwenu, na yule mwenye kumfanyia wema mkewe.”[204]

Akasema (s.a.w.w.): “Tabia njema ni nusu ya dini.”[205]

Imam Jafar bin Muhammad as-Sadiq (a.s.) amesema: “Aliye na imani kamilifu miongoni mwa waumini ni yule mwenye tabia njema.”[206]

## USHAURI NA KUSHAURIANA

Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s.) amesema: “Atakayeitegemea rai yake ataangamia, na atakayechukua ushauri toka kwa watu atashirikiana nao katika akili zao.”[207]

Akasema tena: “Kuomba ushauri ni njia ya uongofu.”[208]

Imam Jafar bin Muhammad as-Sadiq (a.s.) amesema: “Hakika ushauri hautimii ila kwa mipaka yake, hivyo atakayeutambua kwa mipaka yake utamnufaisha, la sivyo madhara yake juu ya mwenye kuomba ushauri ni makubwa kuliko manufaa yake:

“**Kwanza:** Yule unayemwomba ushauri awe ni mtu mwenye akili. **Pili:** Awe ni mtu huru mwenye dini. **Tatu:** Awe rafiki aliye ndugu. **Nne:** Umjuze siri yako kiasi kwamba iwe kuitambua kwake ni sawa na kujitambua kwake mwenyewe, kisha aifiche siri hiyo.

“Kwani hakika akiwa ni mwenye akili utanufaika na ushauri wake, na akiwa ni mtu huru mwenye dini atajibidiisha katika

[204] *Wasailus-Shia* Juz. 12, Uk. 153, Mlango wa 104, Hadithi ya 24.
[205] *Wasailus-Shia* Juz. 12, Uk. 154, Mlango wa 104, Hadithi ya 27.
[206] *Wasailus-Shia* Juz. 12, Uk. 156, Mlango wa 104, Hadithi ya 34.
[207] *Wasailus-Shia* Juz. 12, Uk. 40, Mlango wa 21, Hadithi ya 6.
[208] *Wasailus-Shia* Juz. 12, Uk. 40, Mlango wa 21, Hadithi ya 7.

kukunasihi, na akiwa ni rafiki aliye ndugu ataificha siri yako pindi utakapomjuza, na utakapomjuza siri yako kiasi kwamba ikawa kuitambua kwake ni kama kuitambua kwako hapo ndipo ushauri utatimia na nasaha kukamilika."[209]

## HAKI ZA WAZAZI WAWILI

Ewe msomaji mpendwa! Tumeshataja baadhi ya mafunzo ya kiislamu yanayomuhusu mtoto ambaye tumemtaja mwanzo wa kitabu, na hapa kimebaki kitu ambacho bado hatujakigusia hadi sasa, nacho ni muhimu sana, hivyo inapasa tuelekeze mtazamo wa kijana huyu katika kitu hicho, nacho ni haki za wazazi wawili ambao wamezichosha nafsi zao kwa ajili ya mtoto huyu, wakavumilia matatizo na maumivu katika njia yake, kuanzia siku za mimba mpaka kuzaliwa kwake, kisha kipindi cha kunyonya hadi kuacha kwake ziwa.

Zaidi ya hapo ni zile taabu alizozivumilia mama peke yake katika kipindi cha malezi, na mali alizozitoa baba juu ya mwanae katika kumlisha na kumvisha, kumuuguza na kumwelimisha na mengineyo, hivyo wao wana haki juu ya mtoto ambazo ni wajibu juu yake kuziheshimu.

Hivyo ewe kijana sikia mafunzo ya dini yako yanayoletwa kwako, hivi ni vifungu vilivyodondolewa toka katika Qur'ani tukufu, habari na Hadithi zilizopatikana kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kutoka kwa Ahlul-Baiti wake (a.s.).

Suhubiana vizuri na wazazi wako na wala usiwakalifishe kukuomba kitu chochote wanachokihitaji, usiwasonye watakapokukera, na wala usiwakemee wakikupiga, na sema nao kwa heshima. Wainamishie bawa la unyenyekevu na wala usiwatazame

[209] *Biharul-An'war* Juz. 72, Uk. 102, Mlango wa 48, Hadithi ya 30.

ila kwa macho ya huruma, wala usinyanyue sauti kupita sauti zao, wala mkono wako zaidi ya mkono wao, na wala usiwatangulie wala kutembea mbele yao.

Wawekee tonge mdomoni kwao iwapo wameshindwa kula, waombee maghofira na swali, funga na hiji kwa niaba yao baada ya kufa kwao, na sema: Ewe Mola Mlezi warehemu kama walivyonilea utotoni. Mkirimu mama yako zaidi kuliko baba yako, kwani bila shaka Mtume wa Mwenyezi Mungu aliambiwa: "Kati ya wazazi wawili ni yupi muhimu zaidi? Akasema: "Ambaye alimbeba kati ya mbavu mbili, akamnyonyesha kwa chuchu mbili, akamlea juu ya mapaja mawili na akamfidia kwa wazazi wawili."[210]

Mtu mmoja akamwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Hakika mzazi wangu wa kike amefikia uzee naye sasa yuko kwangu na humbeba mgongoni na humlisha kwa chumo langu, humkinga na adha kwa mkono wangu, lakini pamoja na hayo simtazami kutokana na kumuonea haya na kumheshimu, je kwa hayo nimemlipa?" Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Hapana, kwa sababu tumbo lake lilikuwa hifadhi yako, chuchu lake lilikuwa kinywesheo chako, unyayo wake ulikuwa kiatu chako, mkono wake ulikuwa kinga yako, alikuwa akifanya yote hayo na hali akitamani uhai wako, na wewe unamfanyia yote hayo na hali unapenda kifo chake."[211]

## UHALIFU NA JINAI

Mpaka hapa ewe msomaji mpendwa tumekutajia sehemu ndogo inayohusu hukmu za kisheria na tabia njema, yale ambayo hayaingii

---

[210] *Mustadrakul-Wasail* Juz. 15, Uk. 182, Mlango wa 70, Hadithi ya 3.
[211] *Mustadrakul-Wasail* Juz. 15, Uk. 180, Mlango wa 70, Hadithi ya 3.

chini ya ibada na tiba ila machache, ni tumedondoa idadi ndogo toka katika Hadithi, na lau tungetaka kukusanya zote basi karatasi hizi haziwezi kutosha Hadithi zilizopatikana katika maudhui hii tu ya ndoa. Tumeacha kutaja nyingi miongoni mwa sifa njema na zile zinazohusiana na hali za utu na mengineyo miongoni mwa milango ya fiqhi, kwa sababu kubainisha mambo hayo kunahitaji nafasi kubwa ya ufafanuzi, na huenda tutakutana na wasomaji wapendwa katika kitabu kingine.

Na sasa tunaanza kutaja baadhi ya mambo miongoni mwa kanuni za adhabu za kiislamu, ili utambue kwamba hakika dini ya Uislamu ni dini kamilifu isiyo na upungufu, na kwamba haijaacha chochote ila imekiwekea adhabu na hukmu, hapa tunakutajia muhtasari tu wa vifungu hivyo, visome na kisha utazame kanuni za adhabu za nchi yako, bila shaka utaona kuna tofauti kubwa kati yake kama tofauti ya Mashariki na Magharibi.

Natamani ningejua ni kipi kingewadhuru watawala na viongozi wa nchi za kiislamu lau wangefuata kanuni za Uislamu katika nchi za kiislamu!! Hivi wanahofia kutuhumiwa kwa uhafidhina iwapo watatekeleza sheria za Mwenyezi Mungu?!! Au wanahofia hizaya duniani au adhabu huko akhera, iwapo watafuata kauli ya Mwenyezi Mungu?!! Au wanaona kanuni za Ufaransa (Kimagharibi) na nyinginezo ndio zilizo karibu na usahihi na ndizo zinazofaa kufuatwa kuliko kanuni za mbinguni ambazo zimeteremshwa na Mwenyezi Mungu katika moyo wa Mtume wa Uislamu Muhammad (s.a.w.w.)?!!

Kisha tujiulize: Hakika wakati tulionao ambao kanuni za Uislamu zimetengwa na kuachwa, na zimechukuliwa na kufanyiwa kazi zile kanuni zilizoanzishwa na walevi wa huko Paris, je dola za kiislamu zimenufaika na kanuni hizo? Na je yapo katika kheri, mafanikio, raha na amani yale mataifa ya kiislamu yanayoishi chini ya kivuli cha

kauli za manaswara? Je katika mataifa hayo hakuna mauwaji wala unyang'anyi? Hakuna baa la njaa wala ughali wa maisha? Je hakuna ujinga wala ufakiri, maradhi wala ugaidi, magereza wala unyongaji? Bali ni wema mtupu uliowaenea wote na ustaarabu uliowatosheleza wote, je hali ni hiyo?!!!

Wanasema: Ni vigumu sana kwa watawala wa nchi za kiislamu kuzuia uingizaji wa pombe na bidhaa zake katika nchi za kiislamu, wakidai kwamba uzuiaji wa kuingiza pombe una madhara juu ya hazina kuu ya taifa na uchumi wa dola, kwa sababu serikali itapoteza kodi za pombe toka kwa waingizaji na wauzaji ambao wana leseni inayowaruhusu kuuza pombe!!

Hivi serikali zinatambua kwamba kodi zinazokusanya toka kwa walevi huongezewa juu yake mamilioni ya pesa mfano wake kisha yote kwa ujumla hutolewa na kutumika katika kuanzisha vituo vya vichaa, hospitali za magonjwa ya akili? Ndio, hakika vituo vya vichaa ndio hatua ya mwisho ya walevi, ndio marejeo ya mwisho ya wadau wa pombe. Kisha hutumika maradufu ya mali hizo zilizokusanywa (kutokana na kodi) katika kuanzisha hospitali za wale waliopatwa na ugonjwa wa kifua kikuu, gonjwa hilo angamizi ambalo liko imara kwa ajili ya kuwalipa walevi.

Usiulizie uhalifu, jinai, majanga na hasara ambazo huletwa na walevi, ndege nyingi ambazo huanguka na kupoteza roho za abiria mara nyingi tunamkuta rubani wake alikuwa amelewa, na katika ajali nyingi za magari utakuta ni pombe ndio iliyoichanganya akili ya dereva. Hivi je kodi zinazokusanywa toka kwenye pombe zinaziba na kufidia madhara haya mabaya ambayo yameenea nchi nzima?!!

Kisha tuyatazame magereza, tunayakuta yamejaa na kusheheni wezi, vibaka na wahalifu wengine, je jinai za uuwaji na wizi zimepungua? Au zinazidi kuongezeka siku baada ya siku. Sababu

yake iko wazi, kwani muuwaji anatambua fika ni jinsi gani ataiokoa nafsi yake kwa mali, na mwizi anajua ni jinsi gani atajiokoa kwa rushwa, na wahalifu wa makosa mengine wanajua ni jinsi gani watajiokoa kwa pesa, na hapo ndipo kila uhalifu unakuwa mwepesi kwa yule anayetaka kuutenda.

Lakini lau muuwaji angejua fika kwamba akiuwa atauwawa, na mwizi akatambua kwamba atakatwa mkono wake, na mzinifu akajua fika kwamba atajelediwa mijeledi mia moja, na mlawiti akaamini fika kwamba atauwawa na kuchomwa moto, na wale wenye kujiunga na makundi batili ya uharibifu wakajua fika kwamba malipo yao ni kuuwawa au kusulubiwa basi wasingethubutu kufanya uhalifu huo, kwa sababu wao wanaona adhabu ya duniani ipo mbele yao hata kama watakuwa hawaamini adhabu ya akhera.

Ufuatao ni muhtasari tu wa baadhi ya vifungu vya sheria na kanuni za adhabu za kiislamu:

## ADHABU YA ZINAA:

Mwenyezi Mungu amesema: **“Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanaume, basi mpigeni kila mmoja wao mijeledi mia. Wala isiwashikeni kwa ajili yao huruma katika hukumu ya Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na lishuhudie adhabu yao kundi la waumini.” (Sura Nuur: 2)**.

Mzinifu aliyebalehe aliye huru ajuaye hukumu na aliyezini kwa hiari yake, hujelediwa mijeledi mia moja na hali hana nguo, tena kwa pigo la nguvu, lakini hufunikwa uso wake na tupu yake. Mwanamke mzinifu hujelidiwa na hali amekaa na hali amevaa nguo zake.

Zinaa huthibitika kwa ushuhuda wa wanaume wanne waadilifu, ambao wanatakiwa kuthibitisha kwamba walimshuhudia mwanaume na mwanamke wakiwa katika hali ya tendo hilo. Au kwa mzinifu mwenyewe kukiri mara nne, lakini ni pamoja na kuzingatiwa sharti nyingine zilizofafanuliwa katika vitabu vikubwa vya fiqhi.

## ADHABU YA KULAWITI:[212]

Huuwawa mtendaji na mtendewa lakini kwa kuzingatia sharti zilizotangulia.

## ADHABU YA MSAGANAJI, NA KUSAGANA:

Nako ni mwanamke kumwingilia mwanamke mwenzake, kila mmoja kati yao atajelediwa mijeledi mia moja, lakini kwa kuzingatia sharti zilizotangulia.

[212] Yapasa zifahamike vizuri istilahi zifuatazo kwa mujibu wa Sheria ya Uislamu: **Zinaa:** Ni tendo la mwanaume na mwanamke kujamiiana bila kuwepo ndoa kati yao, sawa iwe ni kwa mwanaume kumwingilia mwanamke mbele au nyuma. **Liwati**: Ni tendo la mwanaume kumwingilia mwanaume mwenzake. Hivyo kwa mujibu wa sheria ya Uislamu mwanaume kumwingilia mwanamke sehemu yake ya nyuma si kumlawiti, na hata asili ya neno lenyewe *lawiti* ambalo ni la asili ya kiarabu, kwa mujibu wa Kiarabu chenyewe halimaanishi kuingilia nyuma tu, bali ni lazima mwingiliwaji awe ni mwanaume. Na hata watu wa Sodoma na Gomora ukiwafatilia katika Aya za Qur'ani hawakuwa wakiwaingilia wanawake nyumani kwao, bali walikuwa wakiwaingilia wanaume wenzao, ndio maana Nabii Luti akawaambia: **"Enyi watu wangu! Hawa hapa binti zangu.." (Sura Hud: 78)**. Hivyo iwapo mwanaume atamwingilia mwanamke sehemu zake za nyuma na ikawa hakuna ndoa kati yao basi hiyo kwa mujibu wa Uislamu wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) itabaki kuwa ni zinaa na si liwati, na kama kati yao kuna ndoa basi hiyo haitokuwa zinaa wala liwati. – **Mtarjumi.**

## ADHABU YA UKUWADI:

Kwa mujibu wa istilahi ya sheria ya Uislamu, ukuwadi ni kitendo cha kuwakusanya wanaume na wanawake kwa lengo la kufanya zinaa, au kuwakusanya wanaume kwa lengo la kulawitiana. Hivyo kuwadi atajelediwa mijeledi sabini na tano, lakini ni pamoja na kuzingatia sharti zilizotangulia.

## ADHABU YA KUMTUHUMU MTU KWA ZINAA AU ULAWITI:

Kumtuhumu mtu kwa zinaa au kwa ulawiti ni kama vile aseme: "Wewe ni mzinifu, au wewe ni mlawiti." Au atumie neno lingine linalojulisha zinaa au liwati, kwa mfano aseme: "Ewe mwana wa mzinifu wa kiume, au ewe mwana wa mzinifu wa kike, au si mtoto wa baba yako, au ewe mume wa mzinifu." Mwenye kutuhumu atajelediwa mijeledi themanini, hatovuliwa nguo zake na atajelediwa kwa pigo la katikati. Haya ni kama aliyenasibishwa na zinaa au liwati ni mwislamu, aliye balehe na timamu wa akili, aliye huru na mtawa. Ama akiwa ni mtoto, au mtumwa, au kafiri au mwenye kujidhihirisha kwa zinaa basi hatoadhibiwa kwa Haddi, bali ataadhibiwa kwa Taazizi.[213] ambayo ni adhabu kiwango chake hutolewa na Imam au Naibu wake.

[213] Haddi ni adhabu ambayo kiwango chake kimeainishwa moja kwa moja. Ama *Taazizi* ni adhabu ambayo kiwango chake hakijaainishwa moja kwa moja bali huainishwa na Imam wa zama husika au Naibu wake wa zama husika. – **Mtarjumi.**

## ADHABU YA MWENYE KUMTUSI MTUME, AU MANABII AU MAIMAMU (A.S.):

Ni wajibu atakayemsikia mtu akitenda hilo amuuwe mtukanaji, iwapo tu kufanya hivyo hakutomletea madhara yeye mwenyewe au mali yake.

## ADHABU YA MWENYE KUDAI UNABII:

Kila anaedai unabii wa uongo ni wajibu kumuuwa.

## ADHABU YA MCHAWI:

Mchawi kama ni mwislamu huuwawa, na kama ni kafiri huadabishwa. Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: 'Mchawi mwislamu huuwawa, na mchawi kafiri hauwawi.' Pakasemwa: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni kwa nini mchawi kafiri hauwawi?' Akasema: 'Kwa sababu ukafiri ni dhambi kubwa kuliko uchawi, na kwa sababu shirki na uchawi vimeambatanishwa pamoja.'"[214]

## ADHABU YA MLEVI:

Kila anayetumia kilevi chochote, kwa hiari, aliye balehe, ajuaye uharamisho wake, hujelediwa mijeledi themanini.

[214] *Al-Kafiy* Juz. 7, Uk. 260, Mlango wa adhabu ya mchawi, Hadithi ya 1.

## ADHABU YA MWENYE KUHALALISHA KILEVI:

Atakayekunywa pombe kwa kuitakidi kwamba ni halali ataombwa atubie, akitubia ndipo ataadhibiwa, na kama akikataa kutubu basi huuwawa.

## ADHABU YA MUUZA POMBE:

Mwenye kuuza pombe kwa kuitakidi kuwa ni halali, ataombwa atubu, la sivyo atauwawa, na kama si mwenye kuitakidi kuwa ni halali, huyo ataadhibiwa kwa adhabu ya Taazizi.

## ADHABU YA WIZI:

Mwenyezi Mungu amesema: **"Na mwizi mwanaume na mwizi mwanamke, basi ikateni mikono yao, malipo ya yale waliyochuma. Ndio adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima." (Sura Maida: 38)**.

Mwizi hukatwa vidole vyake vine vya mkono wake wa kulia, na huachiwa kiganja na kidole gumba, kwa sharti kwamba zitimie sharti zote katika tukio hilo la wizi. Miongoni mwa sharti hizo ni: Mwizi awe ni mtu mwenye akili aliye balehe, aliyekusudia kuiba, na kilichoibiwa kiwe ni kitu kilichokuwa kimehifadhiwa na kulindwa kwa kufuli au kufungiwa au kufukiwa, na thamani ya kitu hicho kiwe ni kuanzia robo ya dinari ya dhahabu na kuendelea, na washuhudie hilo mashahidi wawili waadilifu au akiri mwizi mwenyewe.

Akiiba kisha akakatwa vidole vyake kisha akarudia tena kuiba hukatwa vidole vya mguu wake wa kushoto, kuanzia kwenye maungio

ya vidole na huachiwa unyayo ili autegemee katika kutembea. Na kama akiiba mara ya tatu atafungwa mpaka afie gerezani au atubu, na kama akiiba humo gerezani basi atauwawa.

## ADHABU YA UGAIDI:

Mwenyezi Mungu anasema: **"Hakika malipo ya wale wanaopingana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kufanya uovu katika nchi, ni kuuwawa au kusulubiwa au kukatwa mikono na miguu yao kwa kupishana, au kuhamishwa katika nchi. Hiyo ndiyo fedheha yao katika dunia, na katika akhera watapata adhabu kubwa." (Sura Maida: 33)**.

Gaidi ni yule mwenye kuweka silaha waziwazi ili kuwahofisha watu, baharini au nchi kavu, usiku au mchana, mwanaume au mwanamke, katika nchi au sehemu nyingine, yeye huuwawa au kusulubiwa, au hukatwa mkono wake wa kulia na mguu wake wa kushoto, au hupelekwa uhamishoni. Hiari ya kuchagua moja kati ya hayo huwa ni jukumu la Imam (a.s.) au naibu wake.

## MWENYE KUSULUBIWA:

Mwenye kusulubiwa haachwi zaidi ya siku tatu juu ya msalaba wake, kisha hushushwa na huoshwa, hukafiniwa, huswaliwa na huzikwa.

## MWENYE KUFUKUZWA NA KUPELEKWA UHAMISHONI:

Gaidi hufukuzwa nchini kwake, na huandikwa barua kwenda katika nchi aliyokimbilia inayotaka izuiliwe kula naye, kunywa naye na kukaa naye.

## ADHABU YA MWENYE KURITADI:

Murtadi ni yule anayekufuru baada ya Uislamu, naye ana aina mbili: *Murtadi Al-Fitriy*: Naye ni yule ambaye kazaliwa na wazazi wawili waislamu, au mmoja wao ni mwislamu. Huyo ni wajibu kumuua, na mkewe hujitenga naye kwa talaka ya *baini*, na hukaa eda ya kufiwa, kisha huolewa apendapo. Mali zake (murtadi) hugawanywa baina ya warithi wake, hii ni kama murtadani  ni mtu mwenye akili timamu, aliye balehe na mwenye kufanya hivyo kwa hiari yake.

Na wa pili ni yule *Murtadi Al-Miliy*, naye ni yule aliyesilimu toka katika ukafiri kisha akaritadi, huyu huombwa atubu, akikataa huuawa.

## ADHABU YA KUMWINGILIA MNYAMA:

Lau mtu timamu aliye balehe akimwingilia mnyama aliye halali kuliwa nyama yake, ni wajibu kumwadhibu mwingiliaji kwa adhabu ya Taazizi, na kulipishwa gharama ya mnyama. Na ni wajibu mnyama huyo kumchinja kisha kumchoma kwa kumteketeza.

## KUJITETEA NA KUJILINDA:

Inaruhusiwa kwa mwanadamu kujitetea na kujilinda yeye, familia yake na mali yake dhidi ya mvamizi au mwizi, kwa kadiri awezavyo, kwanza kwa kuchukua tahadhari kisha kwa kupiga kelele, kisha kwa mkono, kisha kwa fimbo, na iwapo hatua hizo hazitomsaidia ndipo atumie silaha, na hapo damu ya mwizi au mvamizi haitokuwa na fidia, na huyu mwenye kujitetea kama atauwawa hapo ujira wake utakuwa sawa na ule wa mtu aliyekufa katika njia ya Mwenyezi Mungu.

# KISASI:

Mwenyezi Mungu amesema: **"Mna uhai katika kisasi." (Sura Baqara: 179)**.

Kila atakayemuuwa moja kwa moja mtu, kwa kukusudia na hali ni timamu, na kafanya hivyo kwa dhulma, na akawa amemuuwa mwenzake kwa kumchinja au kumnyonga, au kwa kumpa sumu iliyomuuwa, au kwa kumpiga na upanga au kisu au jiwe au risasi, au kamchimbia njiani shimo lenye kina kirefu, au akamtupia baharini akaliwa na papa, au kamtupia katika moto akaungua, au akamwamrisha mbwa akamuuwa, na mfano wa hayo, basi ni lazima kumlipiza kisasi kwa sharti tano:

**Kwanza:** Muuwaji na muuliwa wawe sawasawa katika dini, hivyo mwislamu hauwawi kwa kumuuwa kafiri, lakini kafiri huuwawa kwa kumuuwa mwislamu.

**Pili:** Wawe sawasawa katika utumwa na uungwana, hivyo muungwana huuwawa kwa kumuuwa muungwana, na mtumwa huuwawa kwa kumuuwa mtumwa, na mtumwa huuwawa kwa kumuuwa muungwana, lakini muungwana hauwawi kwa kumuuwa mtumwa.

**Tatu:** Muuwaji asiwe ndio baba wa muuliwa, ikiwa baba atamuuwa mwanae hatouwawa.

**Nne:** Awe timamu wa akili, hivyo mwendawazimu hauwawi, bali fidia huthibiti kwa wanafamilia wake wa upande wa baba yake.

**Tano:** Muuliwaji awe ni yule ambaye damu yake imehifadhiwa kisheria, kwa maana asiyeruhusiwa kuuwawa kisheria, hivyo hakuna uharamu wa kumuuwa murtadi, mwizi, gaidi, kibaka na mfano wao iwapo sharti zimetimia.

Fidia ya kuuwa kwa makusudi ni ngamia mia moja, au ng'ombe mia mbili, au mbuzi elfu moja, au dinari elfu moja za dhahabu, au dirhamu elfu kumi za fedha, au ….mia mbili.

Mawalii wa muuliwaji wana hiari ya kuchagua baina ya kisasi dhidi ya muuwaji au kuchukua fidia toka kwake.

Na pia kisasi hupatikana katika kukata sikio, kung'oa jicho, kukata mkono au mguu, au kukata ulimi, Mwenyezi Mungu amesema: **"Na humo tuliwaandikia ya kwamba mtu kwa mtu na jicho kwa jicho, na pua kwa pua, na sikio kwa sikio, na jino kwa jino……" (Sura Maida: 45)**.

## AINA ZA UHAI

Kinachopatikana toka katika Aya za Qur'ani na habari na Hadithi za Mtume na Ahlul-Baiti ni kwamba Uislamu umegawa uhai wa mwanadamu katika aina tatu:

**Aina ya kwanza**: Uhai wa dunia, nao ni pindi roho inapokuwepo katika mwili wa mwanadamu, na tayari katika kitabu hiki tumetaja sehemu ndogo tu ya yale yanayohusu uhai wa mwanadamu katika aina hii ya uhai.

**Aina ya pili**: Uhai wa baada ya kifo, yaani kuanzia siku ya kifo mpaka siku ya kiyama, na huu huitwa Ulimwengu wa Barzakhi, nao ndio mpaka tenganishi kati ya muda wa ulimwengu wa dunia na ulimwengu wa Akhera.

Mwenye kumtii Mwenyezi Mungu atakuwa ni mwenye kuneemeshwa katika ulimwengu wa Barzakh, kwa mwili wake na roho yake humo kaburini, kama ambavyo muasi ataadhibiwa kaburini kwa mwili wake na roho yake.

Hivyo kuanzia hapa Uislamu unazingatia kwamba kifo ni safari ya kuhama toka ulimwengu mmoja kwenda ulimwengu mwingine, na wala hauzingatii kuwa kifo ni kuisha na kutoweka, na kwa ajili hii ndio maana ukaamuru kuuheshimu mwili baada ya kifo, na wala hausemi kuwa wenyewe ni kitu kisicho na uhai, kwa sababu hubakiwa na sehemu fulani ya uhai au roho, japokuwa sisi hatuhisi hilo.

Maana hii tunaipata toka katika mkusanyiko wa Hadithi na adabu zilizopatikana zikihusu kumwandaa maiti, kuanzia hali ya kutoka roho, kumwosha hadi kumzika. Zenyewe zinatamka wazi kwamba maiti huona na kusikia, huhisi na kutambua, na kwamba kaburini ataulizwa kuhusu Mola wake, Nabii wake na Maimamu wake. Na kwamba kaburi huzibana baadhi ya maiti zilizokuwa zikiasi, na huwakamua na kuwagandamiza. Zifuatazo ni baadhi ya hukmu ambazo humo tunaipata maana hiyo iliyotajwa:

Katika hali ya kutoka roho, kuoshwa na kukafiniwa, yapasa maiti afanyiwe upole. Afikishwapo kaburini hufunguliwa vifungo vya sanda kichwani, na maiti hupigwa begani na kuambiwa: "Ewe Fulani bin Fulani…." Na katika dua ya kumwombea maiti husemwa: "Ewe Mwenyezi Mungu unga upweke wake na muondolee woga wake."

Maiti huwekwa karibu na kaburi kisha huvutwa subira kidogo, kisha husogezwa kidogo, kisha kuvutwa subira kidogo, kisha huwekwa katika mdomo wa shimo na kuteremshwa humo. Mtu mmoja alimuuliza Imam Al-Baqir (a.s.): "Ni kwa nini mtu anapokufa huwekewa kijiti cha mtende?" Imam (a.s.) akajibu: "Ili adhabu na hesabu ijitenge naye maadamu kijiti bado kibichi, na hakika adhabu na hesabu vyote huwa siku moja na saa moja, kadiri aingiavyo kaburini na warejeavyo watu…."[215]

[215] *Man'layahdhuruhu Al-Faqiih* Juz. 1, Uk. 145, Mlango wa kuweka vijiti viwili, Hadithi ya 407.

Na katika habari nyingine ni kwamba mpagani alimuuliza Imam as-Sadiq (a.s.: ): "Nieleze kuhusu taa inapozima mwanga wake huenda wapi?" Imam akasema: "Huenda na wala haurudi." Mpagani akasema: "Kwa nini unakataa mwanadamu kuwa si kama hivyo, anapofariki na roho yake kuachana na mwili haitorejea tena, kama ambavyo mwanga wa taa haurejei inapozimika?"

"Imamu (a.s.) akasema: "Ulinganishi haujapatia, hakika moto umo katika viwiliwili vya vitu, na viwiliwili vinajitegemea vyenyewe kama jiwe na chuma, vinapogongana hutoka moto kati yake ambao hufanywa taa yenye mwanga, na moto huendelea kuwepo katika viwiliwili hivyo lakini mwanga huondoka."

Kisha Imam (a.s.) akasema: "Roho ni kiwiliwili chembamba, kimevishwa vazi zito, nalo si kama taa uliyoitaja, hakika ambaye aliumba katika tumbo la uzazi mimba kutokana na maji safi, na akaiwekea aina mbalimbali za mishipa na neva, meno, nywele, mifupa na mengineyo, ndiye atakayemuhuisha baada ya kifo chake, na kumrudisha baada ya kutoweka."

Mpagani akasema: "Roho iko wapi?" Imam (a.s.) akasema: "Mikononi mwa Malaika ambaye ameishikilia mpaka itakapoiaga ardhi." Akasema: "Je roho baada ya kutoka kwenye vazi lake huyayuka?" Imam (a.s.) akasema: "Hubakia mpaka pale parapanda litakapopulizwa…"

Na kuna kundi la Hadithi mutawatiri zinazothibitisha kwamba maiti hutambua vitu, kati ya hadithi hizo ni:

Katika mazishi ya Fatima binti Asad ni kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipiga kofi kwa mikono yake miwili kisha akasema: "Naapa kwa Yule Ambaye nafsi ya Muhammadi imo mikononi

mwake, hakika amesikia Fatima mkono wangu wa kulia ulivyopiga kwenye mkono wangu wa kushoto."[216]

Imamu Amirul-Muuminina (a.s.) alipita pembezoni mwa miili iliyouawa katika Vita vya Jamal huko Basra, akaanza kuisemesha miili ya Talha na Kaab bin Suur na mingineyo, ndipo baadhi ya Sahaba zake wakamuuliza: "Unawasemesha Talha na Kaab baada ya kuuawa kwao?" Akasema (a.s.): "Wallahi wamesikia maneno yangu kama watu wa kisima cha Qalib walivyosikia maneno ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) siku ya Badri."

Ifuatayo ni Hadithi nyingine nayo ni mashuhuri kwa wote, imetajwa pia ndani ya vitabu: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: "Kaburi ima liwe kiunga miongoni mwa viunga vya pepo au liwe shimo miongoni mwa mashimo ya moto." Hakika Hadithi hii inatamka wazi kwamba maiti huneemeshwa au kuadhibiwa kaburini mwake, na huenda ikawa vigumu wewe kuamini Hadithi hii, na nafsi yako inakwambia mara nyingi umeona makaburi lakini hujaona humo maua wala majivu, hivyo vipi yatakuwa ni kiunga au shimo?

Tunakwambia: Ni lazima kusema kwamba majini wapo, kama ambavyo Qur'ani imetamka hilo sehemu mbalimbali za Qur'ani, na jinni humwona mwanadamu na wala mwanadamu hamwoni jinni ila kwa nadra, na wao hula, hunywa na kustarehe, kama Qur'ani ilivyotamka hilo, hivyo ikisihi katika ulimwengu huu tunaoishi bali katika miji yetu na makazi yetu kuwepo viumbe vinavyoishi, vinavyokula na kunywa lakini pamoja na hayo sisi hatujaviona wala kusikia sauti yao, basi ni kipi kizuizi cha roho na miili nayo kuwa hivyo (kutoonekana) na hali inastarehe au kuadhibiwa kaburini? Hivyo haipasi ulimwengu wa kiroho na

[216] *Amalis-Swaduq*, Baraza la hamsini na moja, Uk. 258, Hadithi ya 14. *Biharul-An'war* Juz. 78, Uk. 350, Mlango wa 53, Hadithi ya 22.

ulimwengu wa baada ya kifo kuulinganisha na ulimwengu wa mada.

## MAREJEO

Aina ya tatu ya uhai ni uhai wa Akhera, Qur'ani Tukufu imeutamka wazi, Mwenyezi Mungu amesema: **"Na hayakuwa maisha haya ya dunia ila upuuzi na mchezo, na nyumba ya Akhera ndiyo maisha hasa, laiti wangelijua." (Sura Ankabut: 64)**.

Akasema tena: **"Atasema: Laiti ningelitanguliza kwa ajili ya uhai wangu." (Sura Al-Fajri: 24)**. Na nyinginezo miongoni mwa Aya tukufu ambazo zinaashiria maudhui hii.

Muhtasari wa maneno kuhusu ulimwengu huu wa Akhera ni kwamba mwanadamu atahuishwa mara ya pili akiwa na roho ileile na mwili uleule na viungo vilevile. Huenda pakasemwa: Hakika matendo na maovu ayatendayo mwanadamu duniani hujichora yote katika viungo vyake kiasi kwamba viungo hivyo vitatoa ushahidi dhidi ya mtu muasi:

**"Siku hiyo tutapiga muhuri juu ya vinywa vyao, na mikono yao itatuzungumzisha na miguu yao itatoa ushahidi kwa yale waliyokuwa wakiyachuma." (Sura Yasin:65)**. Tena akasema: **"Nao wataziambia ngozi zao: Mbona mnatushuhudia? Zitasema: Mwenyezi Mungu aliyekitamkisha kila kitu ndiye ametutamkisha." (Sura Fussilat: 21)**.

Kulihali, hakika dini ya Uislamu inamzingatia mwanadamu ni mwenye kudumu, kwa maana kwamba hatoisha na kutoweka moja kwa moja, bali atabaki, kwani watu wa peponi ni wenye kudumu humo, na watu wa motoni ni wenye kudumu humo ila pale shafaa ya

mawalii wa Mwenyezi Mungu itakapowapata ndipo watakapotolewa motoni, ama makafiri wapinzani wao watadumu katika adhabu milele bila kikomo.

Hapana shaka kwamba Mada ya Marejeo ni ya kale, na hapo kabla kulikuwa kukitokea malumbano, mizozo na mijadala baina ya upande wa Manabii na wanatauhidi na ule wa Mazandiki na wapagani, na bado inaendelea mpaka leo. Na lau tukizirejelea Aya za Qur'ani tutazikuta zinazungumzia zaidi marejeo, mkusanyiko, mtawanyiko, pepo na moto kuliko inavyozungumzia maudhui nyingine, na hilo linaonyesha umuhimu wa maudhui hii.

Qur'ani tukufu imetaja baadhi ya kauli za wakanushaji wa uwepo wa marejeo, na ikawajibu kwa kusema: **"Je, mwanadamu hatambui kuwa tumemuumba kwa tone la manii? Lakini amekuwa mgomvi dhahiri. Na akatupigia mfano na kusahau umbo lake, akasema: Nani atakayeihuisha mifupa na hali imesagika? Sema: Ataihuisha Aliyeiumba mara ya kwanza, naye ni Mjuzi wa kila kuumba." (Sura Yasin: 77 - 79)**. Akasema tena: **"Je, mtu anafikiri kuwa sisi hatutaikusanya mifupa yake? Kwa nini? Tunaweza kuzisawazisha ncha za vidole vyake. (Sura Qiyaama: 3 - 4)**.

Hakika wewe lau ukitazama misitari ya vidole vyako, misitari hiyo ya mviringo, na utatambua kwamba mistari ya vidole vya kila mwanadamu inatofautiana na mistari ya mwanadamu mwingine, hivyo duniani hamna watu wawili ila mistari ya vidole vyao inatofautiana. Hivyo Mwenyezi Mungu atakapovifufua viumbe vyake Siku ya Kiyama na kukusanya viungo vyao vilivyotawanyika vilivyosambaa bara, baharini na hewani kisha akawaumba kama walivyokuwa duniani, bila shaka kadhalika atarudisha mistari ya vidole vyao na nakshi za mikono yao. ametakasika Yule Mwenye kuwapa wafu uhai, Mwenye kuwafufua toka kaburini.

Ewe msomaji laazini! Hakika kuna aina nyingine ya uhai wa mwanadamu, nao ni ule uhai ambao jina lake ni baada ya kifo chake, na kubakia utajo wake baada ya kifo chake muda wote na miaka yote, na bila shaka Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameashiria uhai huo kwa kauli yake: "Hajakufa aliyekufa yule aliyeacha nyuma yake moja kati ya mambo matatu: Elimu ambayo watu wananufaika kwayo au sadaka yenye kuendelea au mtoto mwema anayemwombea maghufira." Kama ambavyo Qur'ani pia imegusia uhai wa namna hii, nao ni athari njema aziachazo mwanadamu baada ya kifo chake: **"Kwa hakika sisi tunawahuisha wafu, na tunayaandika waliyoyatanguliza na nyayo zao, na kila kitu tumekihifadhi katika daftari lenye kubainisha." (Sura Yasin: 12)**.

Mpaka hapa tunakomea kutaja machache miongoni mwa mifano ya hukumu za kiislamu, na tunamwomba Muumba awaneemeshe waislamu na awaongoze kuelekea katika yale yenye manufaa na dini yao ambayo amewaridhia kwayo, awazindue toka katika usingizi wa mghafala, awaokoe toka katika maangamizi ya ujinga na awafanye watendaji wenye kutenda kwa ajili ya kuihudumia dini, hakika Yeye ndiye Mwafikishaji bora na Msaidizi bora. Na kila sifa njema kuanzia mwanzo hadi mwisho ni ya Mwenyezi Mungu.

Karbala Tukufu
Sayyid Muhammad Kadhim Al-Qazuwiniy

# BIBIOLOJIA


- *Qur'ani Tukufu*.
- *Amali* cha Saduq, chapa ya Lebanon, Beirut, Mwaka 1400 A.H.
- *Amali* cha Tusiy, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1414 A.H.
- *Biharul-An'war*, chapa ya Lebanon, Beirut, Daru Ihyait-Turathil-Arabiy, Mwaka 1403 A.H.
- *Tuhaful-Uquul*, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1404 A.H.
- *Tahdhibul-Ahkam*, chapa ya Iran, Tehran, Mwaka 1405 A.H.
- *Thawabul-Aamal*, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1400 A.H.
- *Al-Khiswaal*, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1403 A.H.
- *Safinatul-Bihar*, chapa ya Iran, Mwaka 1355 A.H.
- *Uyunu Akhbarur-Ridha*, chapa ya Lebanon, Beirut, Mwaka 1402 A.H.
- *Qurubul-Isnad*, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1413 A.H.
- *Al-Kafiy*, chapa ya Iran, Tehran, Mwaka 1407 A.H.
- *Kamiluz-Ziyarat*, chapa ya Najaf Tukufu, Mwaka 1356 A.H.
- *Majmaul-Bahrayni*, chapa ya Lebanon, Beirut, Mwaka 1403 A.H.

- *Mustadrakul-Wasail*, chapa ya Iran, Qum, Muassasatu Ahlul-Baiti, Mwaka 1408 A.H.

- *Maalis-Sibtwayni*, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1409 A.H.

- *Maanil-Akhbari*, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1379 A.H.

- *Makarimul-Akhlaq*, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1408 A.H.

- *Man'layahdhuruhu Al-Faqiihu*, chapa ya Iran, Qum, Mwaka 1404 A.H.

- *Wasailus-Shia*, chapa ya Iran, Qum, Muassasatu Ahlul-Baiti, Mwaka 1412 A.H.

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia

18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)

61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)

82. Urejeo (al-Raja’a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur’ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu

104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi

126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)

147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia

169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake

190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al- Muraja’aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura

211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi

212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza

213. Imam Ali na Mambo ya Umma

214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa

215. Kuvunja Hoja Iliyotumika Kutetea Uimamu wa Abu Bakr

216. Mfumo wa Wilaya

217. Vipi Tutaishinda Hofu?

218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo

219. Maeneo ya Umma na Mali Zake

220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)

221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala

222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique